Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA NANE

**Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 9 Februari, 2010**

*(Mkutano ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa mezani na:-

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA)**

Taarifa ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira Kuhusu Athari za Mazingira katika Mgodi wa *North Mara.*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 130

### Kitongoji cha Samwa kuwa Kijiji na Kujengwa Zahanati

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika Wilaya ya Kigoma Vijijini kuna Kijiji cha Manyange na Kitongoji kimoja cha Samwa kilicho kilomita 8 na kilicho na wakazi 850 pamoja na Shule za Msingi, lakini hakuna zahanati wala barabara licha ya Sera ya Serikali kutaka kila Kijiji kuwa na zahanati. Kwa kuwa kikao cha Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma kilipeleka taarifa TAMISEMI kuomba kupatiwa Kijiji ili wananchi wa Kitongoji hicho wapatiwe zahanati:-

(a) Je, kwa nini wasipatiwe kijiji kwa kuwa wapo wananchi wapatao 850 na wanayo shule?

(b) Je, kwa nini Serikali isiwajengee zahanati mbali ya kutokuwa na kijiji ili kuondokana na shida wanayopata wagonjwa na akina mama wa Kitongoji hicho?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sijapata F. Nkayamba, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, maombi ya kusajili vijiji huletwa Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI baada ya kupitia michakato mbalimbali ikiwemo maombi hayo kujadiliwa na Halmashauri za Vijiji na Mkutano Mkuu wa Vijiji husika, Kamati za Maendeleo za Kata na hatimaye kupitishwa na Baraza la Madiwani. Baada ya maombi hayo kuwasilishwa, watalaam huyachambua maombi hayo kwa kuzingatia vigezo vilivyoainishwa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi yangu imepokea maombi ya kuanzishwa kwa kijiji cha Samwa. Maombi haya yanaendelea kufanyiwa kazi pamoja na maombi mengine yaliyopokelewa. Naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa kama maombi hayo yatakidhi vigezo, kijiji cha Samwa kitasajiliwa na kuingizwa katika Gazeti la Serikali litakalochapishwa kabla ya Uchaguzi Mkuu wa mwezi Oktoba, 2010.

(b)Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM) imeanza kupeleka fedha katika Halmashauri zote kwa ajili ya kujenga, kupanua na kukarabati vituo vya kutolea huduma za afya kuanzia mwaka 2008/2009. Mpango huu ni mwendelezo wa *Joint Rehabilitation Fund (JRF)* uliomaliza muda wake Juni, 2008.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2008/2009, Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma ilitengewa kiasi cha shilingi 477,825,226/= kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi. Hadi Juni, 2008/2009, shilingi 163,335,580/= zilipelekwa katika Halmashauri hiyo. Kutokana na kuendelea kupatikana kwa fedha zilizokusanywa mwishoni mwa mwaka wa fedha na pia wahisani kutoa fedha walizoahidi, jumla ya shilingi 433,339,103/= zilipokelewa kwa ajili ya kukarabati zahanati na vituo vya afya na pia kununua vifaa na samani katika Halmashauri hiyo ili kuboresha hali ya afya.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maamuzi ya Serikali za Mitaa kujipangia kwa kufuata vipaumbele vyake kwenye matumizi ya fedha, namshauri Mheshimiwa Mbunge awasilishe ombi hilo kwenye vikao vya Halmashauri ili liweze kufikiriwa watakapopata kijiji. Vikao vya Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma ndivyo vinavyoamua kama kuna umuhimu wa kupeleka zahanati katika kitongoji cha Samwa.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuu. Kwa kuwa Serikali inafanya mchakato kwa ajili ya kukipa kitongoji cha Samwa kiwe kijiji, kwa hiyo, hata zahanati nadhani itafuatia mkondo huo huo. Kwa hiyo, naishukuru Serikali iweze kundelea na mchakato huo, sina zaidi. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 131

**Vitongoji Vilivyopendekezwa kuwa Vijiji, Wilayani Kondoa**

**MHE. PASCHAL C. DEGERA** aliuliza:-

Kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa ilipendekeza kwa TAMISEMI Vitongoji kadhaaa kwa lengo la kupandishwa kuwa Vijiji; na kwa kuwa hakuna hata Kitongoji kimoja kilichopandishwa.

(a) Je, ni kwa nini Vitongoji vyote vilivyopendekezwa havikupandishwa kuwa vijiji pamoja na kukidhi vigezo?

(b) Kwa kuwa, Waziri Mkuu alipokuwa akijibu swali la Mheshimiwa Lucas Selelii, Mbunge wa Nzega, katika Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 5/11/2009 alimweleza Waziri mwenye dhamana ya TAMISEMI, kuendelea na mchakato wa kupandisha Vitongoji hadhi kuwa Vijiji kwa Halmashauri ambazo Vitongoji vyake havikufanyiwa kazi ikiwa ni pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya kondoa.

Je, Waziri mwenye Dhamana amezingatia kwa kiwango gani maelekezo ya Waziri Mkuu, kuhusu Vitongoji vya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa ilipendekeza Vitongoji vya kupandishwa hadhi kuwa Vijiji. Aidha ni kweli kuwa Vitongoji hivyo vilikuwa vimekidhi vigezo vya kuwa Vijiji. Hata hivyo, wakati wa mchakato wa kuweka Vijiji hivyo kwenye Gazeti la Serikali yalitokea makosa ya kiutendaji hivyo baadhi ya Vijiji katika Mikoa mbalimbali havikuweza kuingizwa katika Gazeti la Serikali lililochapishwa vikiwemo Vijiji vya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa.

Mheshimiwa Spika, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kuwa zoezi la kuhakiki Vitongoji vilivyokidhi vigezo linaendelea na Vitongoji vyote vitakavyokidhi vigezo ikiwa ni pamoja na Vitongoji vya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa, vitaingizwa kwenye Gazeti la Serikali litakaloandaliwa kabla ya Uchaguzi Mkuu utakaofanyika Oktoba 2010.

(b) Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI amezingatia maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu mchakato wa kupandisha Vitongoji kuwa Vijiji ulifanyika na unaendelea kufanyika kwa maombi yanayopokelewa hivi

sasa. Aidha, kama nilivyoeleza katika kipengele (a) Vijiji vya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa vitaingizwa katika Gazeti la Serikali litakaloandaliwa kabla ya Uchaguzi Mkuu Oktoba, 2010.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Naibu Waziri amekiri kwamba mchakato bado unaendelea. Je, Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba kuna haja ya kuongeza kasi ya huo mchakato ili vitongoji vitakavyokubaliwa kuwa vijiji viweze kujiundia Serikali zake kabla ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naelewa anachozungumza Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna haja ya kuharakisha zoezi hili. Labda niliweke vizuri ili liweze kueleweka nini kinachozungumzwa hapa. Hivyo vijiji ambavyo vinaonekana kwamba kwa sababu ya zoezi lenyewe lilivyo kwenda vilidondoka, kwamba havikuingia katika mchakato kwa maana ya uchaguzi uliopita, ndivyo vijiji ambavyo tunavyozungumzia hapa. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI alikwishakutoa tamko kwamba vile vijiji ambavyo tuliona kwamba vimedondoka pamoja na hivi vingine ambavyo vinaombewa ambavyo kwa kweli katika hali ya kawaida vilikuwa vipite, vitaombewa kwa Serikali ili Uchaguzi Mdogo uweze kufanyika kwa ajili ya shughuli hiyo.

Kwa hiyo, nina hakika kwamba Serikali ilikubaliana na rai hii, kazi hiyo itafanyika na itafanyika mapema kwa sababu kuchanganya uchaguzi huu na ule uchaguzi mwingine unaokuja mkubwa itakuwa ni tatizo. Kwa hiyo, nina hakika kwamba tutazingatia hilo analosema Mheshimiwa Degera. Nichukue nafasi hii kumpongeza sana kwa jinsi anavyofuatilia mambo yake. Huyu mzee, pale ofisini silali usingizi, kila siku yuko pale anafuatilia. Nampongeza sana kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

**SPIKA:** Huwa anakujia usiku? *Anyway! (Kicheko)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali la nyongeza. Kwa kuwa huu mchakato wa kupandisha hadhi vitongoji, vijiji kuwa kata umechukua muda mrefu; na kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba hilo zoezi bado linaendelea na ni tatizo la karibu Halmashauri nyingi, tunaomba vitongoji vipandishwe kuwa vijiji. Je, kuhusu Kata, ni lini Serikali itatangaza Kata zote ambazo zimekubaliwa ili tusiulize maswali hapa tena?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, labda nisaidie kidogo hapa, kinachosajiliwa ni kijiji. Kitongoji huwa hakisajiliwi wala Kata huwa haisajiliwi. Kata inaanzishwa na Kitongoji kinaanzishwa, yaani maana yake kikishatimiza vile vigezo vinavyotakiwa, unaanzisha na ndilo zoezi linaloendelea. Vijiji vinakuwa *registered* na ndiyo maana vinamiliki ardhi.

Kwa hiyo, nilikuwa nataka tuelewane hilo. Sasa tunakuja kwenye hizi Kata; Kata ukishasema hii ni Kata, Mheshimiwa Waziri Mkuu akitamka hapa kwamba hii ni Kata, kama

inatangazwa pale labla ya miezi sita kabla ya uchaguzi, lazima uitishe uchaguzi na mumpate Diwani wa eneo hilo. *That is the bottom line!*

Kwa hiyo, ukisema hapa sasa hivi atangaze leo, akawatangazia Kata fulani na Kata fulani na Kata Fulani, Mheshimiwa Hamad akasimama hapa akasema hivi, nani Diwani wake? Utaambiwa itisha uchaguzi!

Mheshimiwa Spika, kinachoendelea ni nini sasa hivi; nichukue nafasi hii kwa sababu hili ni jambo ambalo Wabunge wamekuwa wanaulizia na wana haki ya kuulizia jambo hili. Zoezi hili linakwenda vizuri, linamalizika. Tunachoangalia sasa hivi, na mapendekezo yameishapelekwa Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu zile Kata zote ambazo zinaonekana kwamba zinakidhi.

Kwa hiyo, kinachotuzuia sasa hivi, kwa sababu tunajua Uchaguzi Mkuu unakuja na tunajua kwamba na Majimbo yanaundwa humo humo na Majimbo lazima ujue pia kwamba Kata zake zitakuwa ni zipi. kwa hiyo, tumeamua kwamba sasa kwamba tufanye hilo, lakini tukichunga hilo eneo la sheria kwamba inasema nini, kwamba kama utatamka sasa hivi hapa, akitamka hapa Mheshimiwa Waziri Mkuu, hapa sheria inatuambia lazima tumpate na Diwani wake, ndiyo maana hatuwataji. Lakini zoezi hili limekwenda vizuri na limekamilika, ni hicho kipengele tu cha sheria sasa kilichobaki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ambayo nadhani yametosheleza. *(Makofi)*

Na. 132

**Dhana ya Utawala Bora**

**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI** aliuliza:-

(a) Je, nini maana ya Utawala Bora?

(b) Je, Tanzania inafuata Mfumo wa Utawala Bora?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS - UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bakar Shamsi Faki, Mbunge wa Ole, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kinadharia dhana ya Utawala Bora ni pana sana kwa sababu wataalam mbalimbali wamejaribu kutoa tafsiri ya dhana hii kufuatana na mazingira ya sehemu wanazotoka. Lakini kwa ufupi, Utawala Bora unaweza kuelezwa kuwa ni utaratibu mzuri unaotumika katika kuendesha shughuli za umma. Misingi ya Utawala Bora ni pamoja na mfumo wa Utawala, ambao huendesha shughuli za jamii, taasisi au nchi kwa uwazi, ushirikishwaji, kuwajibika, kuzingatia utawala wa sheria, kuzingatia haki za binadamu, kupeleka madaraka kwa wananchi, demokrasia na kujali masuala ya jinsia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo utawala bora unaelezwa kuwa ni uwiano mzuri wa jinsi raslimali za nchi zinavyoweza kutumika katika kushughulikia masuala ya kitaifa kwa ajili ya kuwaletea maendeleo wananchi bila kujali ubaguzi wa aina yoyote.

(b)Mheshimiwa Spika, ujenzi wa misingi ya utawala bora unaenda hatua kwa hatua na hauna kikomo. Kwa hiyo, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba, Tanzania inaendesha shughuli zake za umma kwa kuzingatia misingi ya utawala bora. Kuwepo kwa utawala bora katika nchi yetu kunajipambanua kwa kuwepo kwa uwazi na uwajibikaji wa Serikali kwa wananchi.

Baadhi ya shughuli zinazofanywa kwa uwazi na Serikali ni pamoja na uandaaji wa Bajeti ya Serikali ambapo mchakato wake huanzia kwa kushirikisha wadau, kufuatiwa na kujadiliwa na Kamati za Bunge na hatimaye kusomwa na kujadiliwa Bungeni, utaratibu wa kutangaza mapato ya Serikali katika vyombo vya habari, kutangaza mgao wa fedha za Serikali katika Wizara na mamlaka za Serikali za Mitaa na utangazaji wa zabuni za Serikali katika vyombo vya habari.

Aidha, Serikali yetu inaendeshwa kwa kuzingatia haki za binadamu kwa kudhibiti na kupiga vita rushwa, kwa kutoa uhuru kwa vyombo vya habari kwa demokrasia ambapo chaguzi mbalimbali zinafanywa kwa uhuru na haki kwa kuzingatia muda wa chaguzi uliopangwa bila kuahirisha.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni mfano wa nchi chache katika Afrika zilizoweza kufanya chaguzi kila baada ya miaka mitano pasipo kuahirisha tangu tupate uhuru.

**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu yake Mheshimiwa Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, kwa kuwa vyama vya Upinzani katika nchi yoyote ile ya Mfumo wa Vyama Vingi ni taasisi ya kusimamia utawala bora. Je, Serikali inachukua juhudi gani za makusudi za kuvilea na kuviboresha vyama vya Upinzani hapa nchini ?

Kwa kuwa uchaguzi ulio huru, haki na ambao hauna malalamiko ni moja kati ya misingi muhimu ya utawala bora; na kwa kuwa msingi huo haujatekelezwa kikamilifu hapa nchini kama unavyotekelezwa katika nchi nyingine. Je, Serikali inasemaje katika kukamilisha utekelezaji wa msingi huu wa utawla bora? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS - UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kufanya kazi kwa karibu sana na Vyama vya Upinzani na ndiyo maana Vyama vya Upinzani vimeendelea kuwa na Wabunge wengi humu ndani bila ya matatizo. Kwa mfano, Serikali ili kuhakikisha kunakuwepo na Vyama vya Upinzani vinavyoendelea na vinafanya kazi zake kwa haki kwa kuendelesha mikutano yake kwa kufuata sheria na taratibu za nchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu chaguzi zinazofanywa, tangu tulipoanza chaguzi za vyama vingi, Serikali yetu imejitahidi kuwa na chaguzi za haki na huru katika miaka yote hii tangu tuanze mwaka 1992.

**SPIKA:** Chaguzi zote watu hulalamika tu, unadhani ukishindwa utakaa tu kimya! *(Kicheko)*

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa na mimi fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, napenda kumwuliza kama ifuatavyo. Moja kati ya vitu muhimu sana katika nchi yoyote ni usimamizi mzuri wa matumizi ya kodi za wananchi; na kwa mujibu wa ripoti ya karibuni ya Waziri wa Fedha, imeonekana kuwa baadhi ya Halmashauri kuna ufujaji wa fedha ambao mpaka sasa umeshindwa kuondoshwa. Je, Serikali inasemaje juu ya jambo hili ambalo linaonekana ni kasoro kubwa katika utawala bora katika nchi yetu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS - UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi wa kodi za wananchi katika Halmashauri kazi hiyo inafanywa kwa kushirikiana na Madiwani wote ambao na sisi Wabunge tupo na inafanywa kwa uwazi na pale palipotokea matatizo, hatua zimekuwa zikichukuliwa. Na ili kuhakikisha kwamba suala hili linafanywa vizuri zaidi na wenzetu wa Upinzani wanaliona kwa ukaribu kabisa, ndiyo maana hata Mwenyekiti anayeshughulikia masuala ya *Local Government* anatoka katika Chama cha Upinzani. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri! Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge. Sasa ni zamu ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Kwa ridhaa ya Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, swali linalofuata litaulizwa na Mheshimiwa Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura. *(Makofi)*

Na. 133

**Halmashauri Kulipwa 25% ya Mapato Yatokanayo na Uwindaji**

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA (K.n.y. MHE. VITA R. KAWAWA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, kwa mujibu wa Sheria, Halmashauri zinazopaswa kulipwa 25% ya mapato yatokanayo na uwindaji pamoja na shughuli zinazoendana na utalii huo; na kwa kuwa ni muda mrefu Halmashauri ya Namtumbo haijapata fedha hizo na inasemekana kuwa Wizara hazijapata fedha ndio imechukua jukumu hilo kwa sasa na iko katika mchakato wa kushughulikia malipo ya mgao huo moja kwa moja kwa Halmashauri.

Je, Serikali imefikia wapi na ni lini itaanza kugawa mapato hayo kwa Halmashauri husika?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, awali kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Vita R. Kawawa, naomba kutoa salaam za pole sana kwa Mheshimiwa Vita R. Kawawa, familia yake, Ndugu na jamaa kwa kufiwa awali na Baba yake ambaye ni Mwasisi wa Taifa hili. Mheshimiwa, Marehe Mzee Rashid Mfaume Kawawa na hivi karibuni, Alhamisi wiki iliyopita kufiwa na Dada yake Habiba. Mwenyezi Mungu aziweke mahala pema roho za marehemu hao wote wawili, ameni.

Mheshimiwa Spika, baada ya salaam hizo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo ni moja kati ya Wilaya 44 zenye maeneo ya uwindaji wa kitalii na ambazo zinastahili kunufaika na mgao wa 25% kutokana na shughuli za uwindaji wa kitalii. Mgao huo wa 25% hutokana na sehemu ya fedha inayopelekwa Hazina kutokana na ada za wanyamapori waliowindwa katika vitalu vilivyopo katika maeneo ya Wilaya husika. *(Makofi)*

Aidha, Wilaya ya Namtumbo ni moja kati ya Wilaya mpya nchini ambayo ilianza kupata mgao wa 25% mwaka wa fedha 2006/2007. Kabla ya maeneo ya Namtumbo kufanywa Wilaya kamili, maeneo haya yalikuwa yananufaika na mgao huo kupitia Wilaya ya Songea.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa sasa inafanya mchakato wa kufanya tathmini kuhusu kiasi cha fedha ambazo zitapelekwa katika Halmashauri za Wilaya zote zinazostahili ambao ni mgao uliotokana na shughuli za uwindaji zilizofanyika kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

Wizara yangu imepatiwa fedha kutoka Hazina kiasi cha shilingi 800,000,000/= ambazo zitagawanywa kwa Halmashauri zote zinazostahili kupata mgao huo na taarifa za mgao huo kulingana na shughuli za uwindaji wa kitalii uliofanyika zitapelekwa katika Halmashauri zote za Wilaya zinazohusika na mgao huo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mgao huo, Wilaya ya Namtumbo itapata jumla ya shilingi 15,378,451.21 kutokana na shughuli za uwindaji wa kitalii zilizofanyika katika mwaka wa fedha 2008/2009.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya kuridhisha ambayo yamepatikana katika Bunge lako. Hata hivyo, nauliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa mara ya mwisho kabisa Wilaya ya Namtumbo ilipata mgao wa fedha zipatazo milioni 5.23 mwaka ule wa 2006, fedha ambazo kwa kiasi kikubwa zilikuwa ni chache ukilinganisha na mwaka uliopita ambazo zilikuwa milioni 11.2. Sasa, hivi ni takriban miaka mitatu Halmashauri hii ya Namtumbo haijapata fedha hizo.

Je, katika fedha hizo ambazo sasa hivi Wizara imepokea ni sawa sawa na miaka hii mitatu (2007, 2008, na 2009) ambazo Halmashauri hii ilikuwa haijapata?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Yale yote yaliyotokea Namtumbo ni sawa sawa kabisa na yale yalitokea kwa majirani zao Wilaya ya Tunduru.

Je, katika harakati hii ya kulipwa fedha Halmashauri ya Namtumbo, itakwenda sambamba na Wilaya ya Tunduru?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Wizara ya Maliasili na Utalii haikupeleka fedha katika kipindi cha mwaka 2007/2008 na kwa kweli si miaka mitatu.

Lakini, tumefanya mazungumzo na wenzetu wa Hazina kwa sababu sisi kama Wizara hupata fedha hizi kwa kweli kama Wakala tu, tunazikusanya, tunazipeleka Hazina na Hazina wanazirejesha kwetu ili tuzipeleke kwenye Halmashauri. Kwa huo mwaka hatukupata kutokana na matatizo ya kibajeti.

Lakini, tumefanya nao mazungumzo, wametuhakikishia kwamba watakuwa na utaratibu wa kulipa kidogo kidogo hizo *arrears* za huo mwaka ambao umerukwa. Kwa hiyo, utaratibu huu utafanyika kwa Wilaya zote ambazo zinastahili kupata fedha hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili; nimhakikishie Mheshimiwa Mtutura kwamba katika hizi milioni 800, Wilaya ya Tunduru itapata na itapata shilingi 14,402,059/=. *(Makofi)*

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa fedha hizi zinachelewa sana kufika katika Halmashauri zile ambazo zina vitalu vya kuwinda wanyamapori.

Kwa nini sasa ili kuepusha ucheleweshaji wa fedha hizi, wawindaji hawa wasiende kulipa kwenye Halmashauri husika moja kwa moja badala ya utaratibu wa sasa wa kulipwa Wizara ya Maliasili na Utalii, kasha zikaenda Hazina, zirudishwe Wizara ya Maliasili na kisha kurudishwa Halamshauri?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, utaratibu huu ni miongoni mwa *system* zinazotumika katika kutunza kumbukumbu za kihesabu za fedha za Serikali. Halmashauri kwa sasa au hao wawindaji sio wakala wa Serikali wa kukusanya maduhuli ya Serikali, ndio maana sisi tunakusanya, tunapeleka. Hata sisi kwenye maeneo mengine ambako pia tunakusanya fedha hizi, tumekuwa tukiomba sana kwamba tutumie, lakini utaratibu uliopo kwa ajili ya kuweka *proper controls*, zinatakiwa zipelekwe Hazina ili ziwekewe kumbukumbu zake sahihi, halafu ndio ziweze kurejeshwa. Lakini kwa sababu ni pendekezo, mimi nalichukulia hivyo, basi tutazungumza ingawa utaratibu ni huo kwa ajili ya *proper accounting* ya *financies* za Serikali.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri swali dogo tu la nyongeza. Halmashauri za Wilaya ya Kasulu ni kati ya Halmashauri zenye vitalu viwili vya kuwinda; nataka kujua Je, katika hizo Halmashauri 40, Halmashauri ya Kasulu imo, maana tangu zamani hatujawahi kupata mgao wa 20% wa vitalu vya kuwindia? Mheshimiwa Spika, naomba *assurance* hiyo.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kimsingi, Wilaya zote ambazo zinastahili kupata mapato haya zitapata. Kitakachofanyika ni kufanya tu ugawanyaji kutegemeana na kiasi tulichopata. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Nsanzugwanko kama nilivyomhakikishia awali kwa sababu yeye ni jirani yangu aliniuliza kabla,

lakini kwa uhakika kwa wananchi wa Kasulu, basi nimhakikishie tena kwamba Wilaya yake itapata na kwa kweli na Wilaya zingine kadri ambavyo fedha zitakavyokuwa zimepatikana.

Na. 134

**Tunduru Kupatiwa Umeme Kutoka Mangaka**

**MHE. MTUTURA ABDALAH MTUTURA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Tunduru kijiografia iko ukanda wa Kusini mwa nchi yetu ingawa kiutawala imekuwa ukanda wa Kusini nyanda za juu; kuwa mradi wa umeme wa *Mnazi Bay* unatambuliwa kuwa "Mradi wa Umeme kwa Mikoa ya Kusini na Mtwara":-

(a) Je, Serikali haioni kuwa ni vema jina la mradi likawa " Mradi wa Umeme gridi ya Kusini"?

(b) Je, kwa nini Tunduru isipatiwe umeme kutoka Mangaka ambako ni karibu ukilinganisha na Namtumbi?

(c) Kama Serikali inaafiki Tunduru kupata umeme kutoka Mangaka. Je, itakubali ushauri kwamba msongo wa umeme utakao kwenda Mangaka uwe na uwezo wa 33kv badala ya 11 kv?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mbunge wa Tunduru, naomba nitoe maelezo ya ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, Tunduru kwa sasa inapata umeme unaozalishwa kwa jenereta zinazotumia mafuta mazito. Jenereta hizo zipo mbili za ukubwa wa KW 400 kila moja. Hivyo basi ni vyema ikaeleweka kwamba suala siyo upatikanaji wa umeme kwa kuwa tayari kuna umeme,i sipokuwa kufikisha umeme ambao ni nafuu zaidi na ambao una nafasi na mazingira mazuri zaidi ya kukabili ongezeka la mahitaji ya matumizi.

Kwa hiyo, mradi wa kupeleka umeme Tunduru kutokea kwenye gridi ni matokeo ya mipango ya muda mrefu ya kufikisha umeme wa *Grid* kwenye maeneo mengi zaidi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mtutura Abadallah Mtutura, Mbunge wa Tunduru, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mradi wa umeme wa *Mnazi Bay* unatambuliwa kama *Mtwara Energy Project* utakaozalisha umeme MW 30, ambao mapaka sasa unasambaza umeme katika mikoa ya Lindi na Mtwara. Jina hili ndilo linalotumika kwenye mikataba na taarifa mbalimbali

za mradi. Kwa upande wa upana wa mradi,utakapokamilikakatika hatua zilizopangawa utafikisha umeme kwenye Wilaya za Ruanga, Newala, Nachingwea, Tandahimba, Masasi yaani maeneo ya mikoa ya Lindi na Mtwara kwa ujumla. Awamu hii ambayo itakamilika mwezi Mei, 2010, itasambaza umeme wa jumla ya *MW 18.*

Kwa kuwa mfumo wa umeme huu unajitegemea kwa maana ya *"mini grid",* Serikali haioni tatizo la kuwa na jina hilo la "Mradi wa Umeme wa Gridi Kusini" analolipendekeza Mheshimiwa Mbunge. Hata hivyo mradi huu umetumia jina la: *"Mtwara Energy Project",* katika hatua zake zote na ni vyema kufanya tathmini ya athari za kubadilisha jina katika hatua hii. Serikali imepokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na itaangalia uwezekano wa kuufanyia kazi.

(b) Mheshimiwa Spika, mpango wa muda mrefu wa umeme unapendekeza kuwa na mikoa ya Mtwara na Ruvuma itaunganishwa katika gridi ya taifa kwa umeme wa msongo wa KV220. Katika mpango huu, Tunduru inaweza kupatiwa umeme kutoka Mangaka kwa mradi wa *MEP*. Njia mbadala ya kufikisha umeme wa gridi Tunduru ni kutokea Namtumbo baadaye mradi wa Makambako-Songea kukamilika.

(c) Mheshimiwa Spika, suala la msongo gani unapaswa kutumika kufikisha umeme eneo fulani linategemeana na tathmini ya kiufundi kwa kuangalia vigezo mbalimbali. Vipo vigezo kadhaa vinavyoangaliwa kuchagua msongo wa umeme unaotumika wakati wa usanifu wa njia za umeme. Kigezo cha kwanza ni chanzo cha umeme utakapochukuliwa, pili ni urefu wa njia ya umeme husika na tatu ni matumizi ya umeme yanayotarajiwa.

Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa umeme wa grid ama wa Mangaka ama kutokea Namtumbo utazingatia vigezo na matakwa ya kitaalam, na pia malengo ya muda mrefu. Ushauri wake utafanyiwa kazi wakati wa kufanya maamuzi na naomba nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa ushauri wake huo.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Spika niishukuru Serikali na Shirika la Umeme *TANESCO* kwa kuimarisha umeme katika Wilaya ya Tunduru hasa Mji ule wa Tunduru. Ambako sasa hivi tuna jenereta za ziada mbili zinazozalisha umeme *KW 750* kila moja pamoja na shukurani hizo nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Tunduru iko katikati ya mradi huu mkubwa wa *Mtwara Corridor.* Kma ilivyo Dodoma kasi ya maendeleo itakuwa kubwa sana hasa barabara hii ya *Mtwara Corridor* utakapo kamilikana kwa kuzingatia kwamba umeme ni nyenzo muhimu sana ya kuongeza kasi ya maendeleo naomba kuiuliza Serikali. Je, itakamilisha lini utaratibu huu wa tathimini ili tuweze kuelewa Tunduru itapata umeme kutokea wapi kati ya Mangaka au Namtumbo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba *Mtwara Corridor* ina miradi mingi ya kimiundombinu *Infrastructural Development Projects.* Na tathimini inayofanywa au inayotarajiwa kukamilika na *TANESCO* inazingatia hii kwamba ukitoka Masasi kwenda Mangaka kupitia pale kwenda Namtumbo na barabara inayojengwa kutokana na *Millennium Challenge Corporation (MCC)* yote hii itapanua kwa kiasi kikubwa

sana eneo lile zima. Kwa hiyo, katika kufanya tathimini hii ambayo tunatarajia tufanye ya umeme utakaohitajika kwa maeneo yote yale, tutazingatia mahitaji makubwa yatakayotokana na miradi hii ambayo italeta mahitaji makubwa ya umeme na vitu vingine vya maendeleo.

Kwa hiyo, naomba nimsihi Mheshimiwa Mbunge kuwa taratibu hizi zinafanywa na kukamilika kwake kunaenda sambamba na kukamilika miradi mingine na utekelezaji wa miradi hii mingine *Mtwara Development Corridor.*

**MHE. ELIATA N. SWITI:** Kwa kuwa Serikali ina mpango mzuri wa kupeleka jenereta Sumbawanga na Nkasi Mkoani Rukwa. Je, ni mpango upi sasa ambao unaendelea kuhusu kupeleka umeme wa Gridi kutoka Mbeya na Uvinza?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa hivi sasa miradi ya umeme ya kupata umeme wa uhakika kwenye Mkoa wa Rukwa na maeneo ya Nkasi aliyoyazungumzia Mheshimiwa Switi. Kwa sasa hivi mipango iliyopo ni ya manunuzi ya jenereta, Ambayo manunuzi hayo yapo kwenye taratibu za kukamilika na oder imekwisha tolewa kwa ajili ya majenereta hayo ya Mpanda, Sumbawanga pia na maeneo ya Kasulu na Kibondo. Kwa hiyo, kusema kweli mpango wa sasa hivi siyo kuleta *grid obviously* kwa uhakika na muda mrefu tunatarajia tunaweza kuunganisha *grid* lakini hiyo miradi ni mikubwa sana.

Kwa hiyo, miradi ya sasa hivi ni hiyo ya kuleta jenereta lakini pia naomba kusema kuwa hivi karibunu *REA* wamekubaliana na Serikali ya Norway kuanza kufanya utafiti wa chanzo cha maji pale maeneo ya Mkoa wa Rukwa. Chanzo ambacho kina uwezo wa kuzalisha *megawatt 10* kama mradi huu ukikubaliwa ni mradi ambao kwa uzalishaji huo utatosha kwa eneo lote lile kusambaza umeme.

Na. 135

**Utekelezaji wa Sera ya kuwawezesha Wananchi Kiuchumi**

**MHE. MBARUK K. MWANDORO** aliuliza:-

Kwa kuwa, wakulima na wajasilimali wadogo hawajaweza hawajaweza kunufaika na sera ya uwezeshaji wananchi Kiuchumi hata kupitia MKURABITA na *SACCOS* na kuwafanya wananchi wakate tamaa na kuona na hata kaulimbiu na mikakati ya KILIMO KWANZA kuwa ni wimbo tu:-

(a) Je, Serikali imefikia wapi kuzishawishi Benki kukubali hati zinazotolewa na MKURABITA kama dhamana ya kuombea mikopo?

(b) Je, ni vipi Benki ya Rasilimali *(TIB)* inaweza kuwasaidia wakulima wadogo?

(c) Je, ni hatua gani zinachukuliwa na Benki ya kilimo inayoundwa pamoja na Benki ya Wanawake na taasisi zingine ziweze kuwasaidia wananchi wanyonge vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbarouk Kassim Mwandoro, Mbunge wa Jimbo la Mkinga, lenye shemu (a), (b) na ( c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, juhudi za kuzishawishi Benki za biashara ili zikubali hati miliki za ardhi za kimila kama dhamana za mikopo inaendelea vizuri na Benki ya *CRDB* imeanza kutoa kwa kutumia hati hizo. Aidha napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kulingana na kanuni za Benki za Biashara zinazotoa mikopo, dhamana ya mikopo ni moja ya kigezo kinachohitajika kabla ya kupatiwa mikopo.

Vigezo vingine ambavyo ni muhimu ni pamoja mchanganuo wa biashara, uwezo wa mkopaji wa kulipa deni analotaka kukopa, uwezo wa mkopaji wa kuendesha biashara, historia ya mkopaji ya kuweka fedha benki pamoja na mwenendo wake wa kulipa deni.

(b) Mheshimiwa Spika, benki ya rasilimali imeshafungua dirisha kwa ajili ya kuwakopesha wakulima. Serikali katika mwaka wa fedha 2009/2010 imetenga shilingi bilioni 22 kwa ajili ya kutoa mikopo ya kilimo.Ili fedha hizo ziwafikie na kuwasaidia wakulima wengi zaidi na hasa wale wadogo walioko vijijini, benki ya rasilimali imeandaa mpango ufuatao:-

(i) Kukopesha fedha kupitia *SACCOS*, VIKOBA, Vyama vya Ushirika, Benki za jamii na vyama vya Wakulima wa nje *(Outgrowers Associations)*. Utaratibu huo wa ukopeshaji umetokana na ukweli kwamba vikundi hivyo ndivyo vilivyo karibu na wakulima.

(ii) *TIB* imejiandaa kufungua Ofisi za kanda ili kuwa karibu zaidi na wakulima.

(iii) *TIB* itatumia wakala wa usambazaji wa zana za Kilimo. Wakala hao watatoa pia mafunzo kwa wakulima pamoja na kupewa jukumu la kufanyia matengenezo vifaa vya kilimo vya wakulima.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa kuwasaidia wananchi wanyonge hasa walioko vijijini, Serikali kupitia Benki ya Kilimo na Taasisi nyingine za fedha iatachukua hatua zifuatazo:-

(i) Serikali itatoa fedha kwa Benki ya Rasilimali ili ukopeshwaji wake uwe wa riba nafuu ambayo ni kati ya asilimia 5 hadi 8 kwa mwaka.

(ii) Mikopo itakayotolewa italipwa kwa kipindi cha kati ya miezi sita hadi 15 kuendana na mahitaji ya mradi.

(iii) Marejesho ya mkopo yatapangwa kuendana na msimu wa kilimo.

(iv) Dhamana itahusisha mali ambazo wananchi wa vijijini wanazo kama vile ardhi, mashine na kadhalika.

(v) Wakulima kabla ya kupatiwa mikopo watasaidiwa kuandaa michanganuo ya biashara.

(vi) Barabara zinazokwenda mashambani zitaboreshwa ili mazao ya mkulima yaweze kufika sokoni kwa urahisi, kwa kufanya hivyo kutamsaidia mkulima mapato mengi zaidi.

(vii) Kupanua miundombinu ya umwagiliaji ili kuongeza uzalishaji ili kuongeza uzalishaji.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa, bado wananchi wengi wanalalamika kuhusu ugumu wa upatikanaji mikopo pamoja na vigezo vyote vilivyoelezwa.

Je, Serikali ina utaratibu wa ku- *check* na kuona kwamba vigezo hivyo vinapotekelezwa wananchi wanapewa bila vikwazo?

(ii) Naipongeza Serikali kwa mipango mizuri na maandalizi mazuri kuhakikisha kwamba wanyonge wanapata mikopo kama ilivyoelezwa.

Je, mipango hii ambayo iko njiani sasa hivi inarajiwa kuanza kutelezwa lini?

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE.OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika kwanza nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge. Kwamba hakutakuwa na kikwazo chochote iwapo mkopaji atakamilisha zile taratibu kwa mujibu wa kanuni na taratibu za kibenki.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie vilevile Mheshimiwa Mbunge kwamba taratibu za wakulima kukopa kupitia *TIB* sisi Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi. Tumeshazikamilisha baada ya kukamilisha *Suplimentary* ya bilioni 19 sasa dirisha lina fedha za kutosha wakulima wanaweza wakaanza kufuta utaratibu, na kuanza kukopa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kiongozi wa kambi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Hamad Rashid.

**MHE. HAMAD R. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ni 10% tu ya Watanzania ndiyo wanaoweka fedha zao Benki. Na kwa mujibu wa maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba moja kati ya sharti la kupata mikopo ni kwamba uwe na mteja ambaye amekuwa akiweka fedha kila wakati katika Benki. Kwa hiyo, Watanzania ambao hawana utaratibu wa kuweka pesa Benki watakuwa hawaingii katika utaratibu wa kupata mikopo kwa sababu hawatimizi masharti, hili mnalitizama vipi kwa Watanzania ambao wengi bado hawakuweka fedha zao benki.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE.OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, kwanza ninakubaliana naye kwamba ni 10% ya Watanzania ndiyo wanaoweka fedha zao benki. Lakini vilevile kama nilivyosema katika maelezo yangu ya msingi kwamba vile ni vigezo siyo masharti.

Kuna tofauti baina ya masharti na vigezo lakini hata hivyo katika maelezo yangu ya msingi nimesema kwamba *TIB* itazikopesha *SACCOS* hawa wakulima wanaweza wakaweka fedha zao *through SACCOS* na wakapata mikopo kupitia *SACCOS.*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, kwanza niishukuru Serikali kwa kufanya mazungumzo na kwamba sasa benki ya CRDB imekubali kutoa mikopo kwa wale wote ambao wana Hati Miliki za Kimila.

Lakini benki ya *NMB* ndiyo yenye mtandao mkubwa sana nchini karibu inafika Wilaya zote hivyo ni rahisi kufikiwa na Wananchi wote, sasa ni lini hasa Serikali itafanya mazungumzo na *NMB* ili ikubali kutoa mikopo kwa wananchi wote ambao wana hati miliki za kimila kwa maana wafaidike na mikopo hii. Na wananchi wa Mbozi ambao ndiyo wa kwanza kabisa waweze kufaidika na zoezi hili.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, katika biashara yoyote kuna kitu wanakiita *Opportunity Cost.*

Kila benki ya biashara wanaangalia uwezekano wa kukopesha na fedha yake kurudi kulingana na taratibu za kibenki Serikali inafanya juhudi hizo kuzungumza siyo na *NMB* peke yake inajitahidi kuzungumza na mabenki yote ya biashara ili yaweze kufanikisha lengo hili, namwomba Mheshimiwa Zambi avute subira maadam *CRDB* wameanza wameshaonyesha njia kwa mabenki mengine ya biashara nina imani kwamba mabenki mengine ya biashara yatafuata.

Na. 136

**Wafanyakazi wa Jamhuri ya Muungano Kutozwa Kodi za Zanzibar**

**MHE. VUAI ABDLLAH KHAMIS** atauliza:-

Kwa kuwa, wafanyakazi wamekuwa wakikatwa kodi kutoka katika mishahara yao ili kuchangia huduma za kijamii pamoja na mambo mengine:-

Je, kwa nini wafanyakazi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walioko Zanzibar wasikatwe kodi za mishahara yao katika sehemu wanazopata huduma za kijamii.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIA S. SUMARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vuai Abdalla Khamis, Mbunge wa Jimbo la Magogoni, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Kodi ya mapato ni kodi ya Muungano na hutozwa kwa Utaratibu wa zuio *( withholding Scheme)* kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Kodi ya mapato sura ya 332. Utaratibu huu unampa mwajiri kukata kodi mahali ambapo Hati ya kutayarisha mshahara wa mfanyakzi *(Payroll)* huandaliwa.

Kwa maana hiyo kama Hati ya malipo hutayarishwa bara kodi ya mapato hukatwa Bara na kuingizwa katika mfuko mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na kama hati hiyo ya malipo hutayarishwa Zanzibar, Kodi ya Mapato hukatwa Zanzibar na kuingizwa katika mfuko mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nina swali dogo la nyongeza. Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa kuna Taasisi sehemu ya kodi ya mshahara inayolipwa Hati zao zinazotengenezwa Zanzibar na kulipwa Zanzibar naomba uziainishe ni taasisi gani.

**SPIKA:** Labda ungerudia hapo kidogo hata mimi sikulipata vizuri tafadhali Mheshimiwa Vuai.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:**Nina sema kuna sehemu gani ya Muungano Hati zao zinazotayarishwa Zanzibar za malipo na kodi zao zikabakia Zanzibar.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE JEREMIA S. SUMARI):** Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Vuai wa Jimbo la Magogoni kwamba sijui.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kwa maelezo ya ziada, Mheshimiwa Omar Yussuph Mzee.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUPH MZEE):** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri napenda kuongezea kama ifuatavayo:-

Mheshimiwa Spika, kiutaratibu kama Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha alivyojibu kwamba pale ambapo mishahara inakotolewa ndipo ambapo inatakiwa ikatwe kodi. Mheshimiwa Mbunge ametaka kujua nitatoa mfano mmoja mfano Kampuni ya *ZANTEL* ambapo Makao Makuu yake yako Zanzibar wanakotoa mishahara yao Zanzibar. Kwa hiyo, ile kodi inalazimika ibakie Zanzibar.

**SPIKA**: Nadhani inatosha jamani ah! Wizara ya Miundombinu swali linaulizwa na Aloyce Kimaro wa Vunjo.

Na. 137

**Uagizaji wa Samani Kutoka Nje ya Nchi**

**MHE. ALOYCE BENT KIMARO** aliuliza:-

Kwa kuwa, kumekuwa na mtindo wa kuagiza samani *(furniture )* kutoka nje ya nchi badala ya kutengeneza za kwetu wenyewekwa kuwa mbao tunazo:-

(a) Je, ni kiasi cha fedha kimetumika kuagiza samani za ofisi na majumbani kwa matumizi ya Serikali kuanzia mwaka 2005- 2008?

(b) Je, Serikali itaacha lini kuagiza samani kutoka nje ya nchi na kutumia viwanda kama vile *SIDO*, JKT, MAGEREZA na kadhalika kutengeneza fenicha tunazotaka?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aloyce Bent Kimaro, Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2005 mpaka mwaka 2008 Serikali ilitumia kiasi cha shilingi 4, 528, 740, 000,00 kwa ajili ya ununuzi wa samani za ofisi na majumbani kwenye maduka yanayouza samani.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali haiagizi samani hizi moja kwa moja kutoka nje ya nchi. Kinachofanyika baada ya kupata mahitaji hutangaza zabuni kwa kutumia sheria ya manunuzi ya 21 ya mwaka 2004. Kwa hiyo makampuni mbalimbali ya kuuza samani hapa nchini huomba na hatimaye huteuliwa na Wizara kuleta samani kwa ajili ya matumizi ya Serikali.

Hata hivyo ili kuweza kulinda wafanyabiashara wa ndani wa samani, Serikali itaendelea kuchukua hatua zifuatazo:-

(i) Kuendelea kutoa elimu kwa watumishi wa umma kupenda kunua samani zinazotengenezwa hapa nchini.

(ii) Kuendelea kutoa maelezo kwa Wizara na Idara za Serikali juu ya kutumia viwango *(Specifications)* vinavyotolewa na Wizara yangu kwa ajili ya ununuzi wa samani.

Mheshimiwa Spika, hatua hii itasaidia taasisi zetu kama JKT, *SIDO* Magereza na kadhalika kuweza kuingia katika ushindani kwa kufuata Sheria ya manunuzi kwa kuuza samani zake kwa Serikali endapo zitakuwa zimekidhi viwango.

**MHE. ALOYCE BENT KIMARO:** Mheshimiwa Spika, baada ya majibu ambayo sijaridhika nayo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

(a)Mheshimiwa Spika, bidhaa zote kutoka nchi za nje hulipiwa kwa kutumia fedha za kigeni. Ambazo tunazo kidogo sana kwa kuwa mauzo yetu nchi za nje ni kidogo. Inakuwaje Serikali inaruhusu fedha zake za Kigeni kutumika kununulia samani ambapo uwezo wa kuzalisha samami hapa nchini na kuongeza ajira upo?

(b)Mheshimiwa Spika, katika swali langu namba (b) iliuliza. Je, Serikali itaacha lini kuagiza samani kutoka nje ya nchi na badala yake viwanda vya *SIDO*, JKT na Magereza swali hili halikujibiwa kwa hiyo sasa lijibiwe Serikali itaacha lini?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika swali la msingi kwamba Serikali haiagizi samani hizi moja kwa moja toka nje ya nchi. Ni biashara mbalimbali au maduka mbalimbali ndiyo yanaagiza bidhaa au samani kutoka nchi za nje iwe ma-*fridge*, iwe *funiture*, iwe kapeti na kadhalika. Kwa hiyo, pesa hizi siyo za Serikali moja kwa moja kwa kuagizia bidhaa kutoka nchi za nje. Kwa maana hiyo ni kwamba pamoja na kuwa Serikali itachukua juhudi za kuhamasisha:-

(i) Viwanda vya ndani vizalishe bidhaa za kutosha.

(ii) Kuhamasisha Idara za Serikali kutumia bidhaa za ndani lakini hakuna njia ambayo tutasema kwamba waagizaji wasiagize kutoka nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, swali la pili linafuatana na swali la kwanza ni kwamba kwa nini Serikali isisitishe kuagiza bidhaa hizi. Ninajibu kwamba si mpango wa Serikali kuweka zuio la mtu yoyote kuagiza bidhaa kutoka nchi za nje.

**SPIKA:** Nadhani tuendelee waheshimiwa Muda ni mgumu kidogo swali linalofuata ni la Miundombinu litaulizwa na Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya.

Na. 138

**Ucheleweshwaji wa Fedha za Barabara ya Kigoma – Nyakanazi**

**MHE. MHONGA SAIDI RUHWANYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika Bajeti ya 2008/2009 tuliahidiwa kuwa barabara ya kigoma Nyakanazi itatengewa fedha kwenye Bajeti ya 2009/2010, bahati mbaya haikutengwa:-

(a) Je, kwa nini Serikali imeshindwa kutimiza ahadi yake?

(b) Je, Serikali haitambui kuwa barabara hiyo ni muhimu sana kwa Uchumi wa Wana Kigoma kwa kuunganishwa na mikoa ya Mwanza, Shinyanga na Kagera?

(c) Kwa kuwa Bajeti ya 2009/2010 ina vifungu kama vile *allowance in kind* vifungu vinavyohusu posho na takrima. Je, kwa nini vifungu hivyo visipunguzwe na fedha hizo kuanza kujenga barabra hiyo ili kuzingatia kipaumbele?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Serikali haijashindwa kutekeleza ahadi zake. Katika kutekeleza ahadi hii ya kujenga barabra kwa kiwango cha lami, Serikali imeanza kujenga barabara hii kwa awamu kutoka Kigoma hadi Kidahwe urefu wa (km36) ambapo mkandarasi *CHICO* kutoka Jamhuri ya watu wa China anaijenga sehemu hii ya barabara kwa kiwango cha lami kwa gharama ya shilingi bilioni 32,543.

Sehemu ya barabara kutoka Kidawe hadi Nyakanazi (km 300) imefanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na kukamilika.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua sana umuhimu wa barabara hiyo kwa Uchumi wa wananchi wa Kigoma kwa kuwaunganisha na Mikoa ya Shinyanga, Mwanza na Kagera. Kwa kuzingatia umuhimu huo Wizara yangu katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2009/2010 imetenga jumla ya shilingi bilioni 1.4 kwa ajili ya matengenezo mbalimbali kwa kiwango cha changarawe ili barabara hiyo iendelee kupitika.

Wakati huohuo Serikali itaendelea na ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami kwa kutumia fedha za ndani na kuendelea kutafuta fedha kutoka kwa washirika wetu wa maendeleo ili kukamilisha ujenzi wa barabara yote.

(c) Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Wizara yangu 2009/2010 iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu, vifungu vya takrima vina fedha kidogo sana kuweza kuanza ujenzi wa barabara.

**MHE. MHONGA SAID RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukiambiwa mara nyingi mambo ya usanifu wa kina, upembuzi yakinifu, barabara itajengwa naomba kujua ni lini barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami? Maana toka Uhuru tunaambiwa barabara itajengwa.

Mheshimiwa Spika, swali la pili sikubaliani na Mheshimiwa Waziri anaposema vifungu vya takrima, *intertaiment*, *allowance in kind* kwamba ni kidogo. Kama swali langu nilivyouliza kwa sababu kwa mwaka jana tu *allowance in kind* ni bilioni 19,milioni 964 na ushee kwa miaka mitano ukizidisha hiyo ni zaidi ya bilioni 998.

Je, kama pesa hizo zingekuwa zikitumika kidogokidgo tusingeweza kujenga barabara zetu kwa pesa zetu za ndani?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi kwamba ahadi hii ni ahadi ya Rais na Rais ni mtu muungwana, anaahidi kile anachotenda na tunatenda kile ambacho Rais amekiahidi, barabara tumeanza kuijenga kutoka Kigoma kwa kilomita 35 kuelekea Kidahwe na tukitoka Kidahwe tunaelekea Nyakanazi haraka iwezekavyo kwa kadri tutakavyopata pesa. Si ahadi tu bali sasa hivi utekelezaji umekwishaanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu vifungu vya *allowances in kind* moja ni *allowance* ambazo zinafanya kazi na hesabu ambazo Mheshimiwa Mhonga amezitoa za bilioni kumi na tisa ni uwezo wa kujenga barabara ya lami usiofikia kilomita kumi na tisa kwa hivi sasa. Kwa hivyo, hakuna njia ambayo tutaacha watalaam ambao wanafuatilia kazi hizo mikoani na kufanya kazi zingine ofisini ambazo zinawezesha utekelezaji wa miradi hii ukategemea kwamba miradi itatekelezwa bila shughuli hizo zinazofanywa kwa siku. (*Makofi*)

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Waziri na nia njema sana ya Serikali, namwomba Waziri kama anaweza akatusaidia watu wa Kigoma kwa mwaka wa bajeti 2010/2011, kwa staili hiyo tuliyoanza ya kilomita 35 kwa nini sasa tusijenge kilomita sitini kutoka pale Kasulu ili taratibu na sisi tuweze kumaliza barabara hiyo?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, ombi nimelisikia na tutalizingatia na kulifanyia kazi katika bajeti inayofuata. (*Makofi*)

**SPIKA**: Ahsante sana, sina budi kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu kwa uungwana wake katika kujibu maswali haya, kwa sababu ni kujaribu kupata majibu bila kuingia katika mapambano na vitu kama hivi, nakushukuru sana. (*Makofi*)

Na. 139

**Bajeti ya Ujenzi wa Bandari**
**ya Kisasa Maruhubi**

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika mipango ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kulikuwa na nia ya kutenga fedha katika bajeti kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya kisasa kwenye eneo la Maruhubi:-

(a) Je, azima hiyo imefikia wapi?

(b) Je, mpango huo unategemea kukamilika lini?

(c) Je, wananchi wajiandae vipi kama mchango wao katika ujenzi huo?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu uliopo ni kwamba nchi mwanachama huwasilisha mradi wake katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na endapo utakubalika kuwa mradi wa kikanda, Jumuiya husaidia katafuta wahisani, wawekezaji au wakopeshaji watakaowezesha mradi husika

kutekelezwa. Iwapo fedha zitapatikana ni jukumu la nchi husika kuingia mkataba na wahisani au wakopeshaji na kusimamia utekelezaji wa mradi husika. Kwa maana hiyo, kama ni mkopo basi jukumu la kulipa mkopo huo si la Jumuiya bali ni la nchi husika. Kwa sasa, Jumuiya haina utaratibu wa kutenga fedha katika bajeti yake kwa shughuli za aina hii. Hata hivyo, kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo tunaandaa utaratibu kwa ajili ya kuchangia miradi ya pamoja.

Mheshimiwa Spika, mradi wa ujenzi wa bandari ya Kisasa ya Maruhubi ni miongoni mwa miradi nane (8) ya Zanzibar iliyopendekezwa kujumuishwa katika programu na miradi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Azma ya kuhakikisha mradi huu unatekelezwa haijabadilika. Wizara iliandaa kikao kilichojumuisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki tarehe 5-6 Novemba, 2008 kwa ajili ya kusaini Makubaliano ya awali (*Aide Memoire*) ya kuanzisha taratibu za kujumuisha miradi nane ya Zanzibar katika programu za Jumuiya ukiwemo mradi wa Maruhubi. Baada ya hatua hiyo sasa Jumuiya inatafuta fedha kwa ajili ya mradi huo na mingineyo.

(b) Mheshimiwa Spika, ukamilikaji wa mradi huu utategemea upatikanaji wa fedha toka kwa wadau wa maendeleo. Kwa hiyo, naomba kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa pale fedha zitakapopatikana tutahakikisha tunaharakisha taratibu za kuwezesha utekelezaji wa mradi huu.

(C) Mheshimiwa Spika, pindi utekelezaji wa Mradi utakapoanza wananchi wajiandae kuunga mkono juhudi zitakazokuwa zikifanyika katika kutekeleza mradi huu.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, kwa kuwa kikao cha mwisho hadi hivi sasa ni karibu miaka mitatu, je, ni nini kinachoendelea?

**SPIKA**: Ahsante kwa swali fupi.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, hivi sasa mchakato wa bandari ya Maruhubi unaendelea na *EU* imeonesha nia ya kusaidia mradi huu, na tayari watalaam kutoka *EU* na watalaam kutoka sekretarieti ya Afrika Mashariki wamekutana huko Zanzibar kwa ajili ya kutafuta fedha za mradi huu. Hata hivyo, inaonekana kwamba, mfuko wa *European Development Fountain* ndiyo utakaoweza kusaidia mradi huu. (*Makofi*)

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika miaka ya 1995 ilikuwa ina nia ya kuanzisha bandari huru na ikaambiwa wakati bado haujafika. Nataka nijue kupitia kwa Mheshimiwa Waziri kwamba bado wakati haujafika wa kuanzisha bandari huru?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, uamuzi wa kuanzisha bandari huru ni wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na hivi sasa wameanzisha mpango maalum wa bandari huru ambao umeshaanza na unafanya kazi. Pale watakapoona tayari wakati umefika kuanzisha bandari huru wanaweza kufanya hivyo.

Na. 140

**Kutumia Vijana Katika Ujenzi wa Taifa**

**MHE. JACKSON M. MAKWETA** aliuliza:-

Kwa kuwa, kujitawala ni kujitegemea na kwa kuwa Watanzania hatujitegemei katika mambo mbalimbali kwa sababu ya kutotumia vizuri nguvu kazi ya watu wetu waishio Mijini na Vijini:-

(a) Je, kwa nini Serikali isibuni miradi mbalimbali kama vile ujenzi wa nyumba za walimu mijini na vijijini, kuchimba mitaro ya maji, mawe, kujenga mabweni na kadhalika, ili kutumia nguvukazi ya vijana wake kwa mtindo wa ujenzi wa Taifa katika ngazi ya kila Wilaya hivyo kutumia fedha kidogo za bajeti kwa njia hizo na kuachana na makandarasi?

(b) Je, Serikali haioni kuwa askari wa JKT, JWTZ, na Mgambo Wastaafu wangeweza kutumika kudumisha nidhamu katika makambi hayo ya muda endapo miradi hiyo itabuniwa?

(c) Je, kwa nini Serikali isitenge mapema maeneo ya kambi hizo kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya ili kuepuka ukosefu wa maeneo wakati utakapofika?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jackson Muvangila Makweta Mbunge wa Njombe Kaskazini lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imepokea wazo zuri la Mheshimiwa Mbunge. Kwa sasa sheria zilizopo ikiwemo ile ya Manunuzi ya Umma haziruhusu utaratibu huo. Lakini napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itatafakari na kulifanyia kazi wazo hili zuri.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali ilipounda Jeshi la Wananchi wa Tanzania JWTZ, Jeshi la Kujenga Taifa na Jeshi la Mgambo ilitoa majukumu ya msingi kwa kila Jeshi yakiwemo ulinzi wa mipaka, kulea vijana, kusaidia mamlaka za kiraia wakati wa maafa, pendekezo la kulinda nidhamu katika makambi ya miradi litakuwa jukumu jipya ambalo makambi hayo yataanzishwa, usimamizi wa nidhamu ufanywe na askari wastaafu kwa kuajiriwa kwa muda.

(c) Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali ikiridhia wazo la kuanzisha kambi hizo mchakato wa kutenga maeneo ya kambi hizo kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya utafanyika mapema.

**MHE. JACKSON M. MAKWETA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Duniani hakuna kinachodumu isipokuwa mabadiliko, pendekezo hili lilitolewa na Rais wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Mkapa na pendekezo la Rais kwa Jeshi ni agizo.

Je, kutokana na hali hii na katika jibu anasema hivi, inashauriwa endapo makambi hayo yataanzishwa usimamizi wa nidhamu ufanywe na askari wastaafu kwa kuajiriwa kwa muda, sielewi inashauriwa wakati agizo hili lilikwishatolewa na kwamba tukichelewa kuchukua ardhi sasa katika Wilaya tutakosa kuwa na makambi hayo ya kulelea vijana wetu ambalo ni jukumu la Jeshi mpaka hivi sasa. Sheria zinatungwa na Bunge na zinaweza kubadilishwa na Bunge. Sasa, je, haoni kwamba kwa lengo la kukidhi nia hii nzuri ya kutumia nguvu kazi ya vijana tungeanza sasa kwa sababu uamuzi ulikwishatolewa?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi ni kwamba kwa taratibu na sheria tulizokuwa nazo sasa jambo hili haliwezi kutekelezwa mpaka sheria hizo zifanyiwe marekebisho. Kama ninavyofahamu Mheshimiwa Makweta mabadiliko ya sheria ni mchakato, nilichosema ni kwamba tunaendelea kulifuatilia agizo hili ili hatimaye hizo sheria ziweze kufanyiwa mabadiliko kwa kufuata mchakato wa kawaida wa ubadilishaji wa sheria ili suala hili liweze kutekelezeka. Jambo hilo tutakuwa tayari kulifuatilia ili wazo hili zuri litekelezeke.

Na. 141

**Ujenzi wa Mahakama za Mwanzo na**
**Nyumba za Mahakimu Korogwe**

**MHE. ENG. LAUS O. MHINA** aliuliza:-

Kwa kuwa, majengo mengi ya Mahakama za Mwanzo katika Kata mbalimbali Jimbo la Korogwe Vijijini yamechakaa sana na mengine hayafai hata kwa matumizi:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuyafanyia matengenezo makubwa au kujenga majengo mapya katika maeneo kama vile Magoma, Vugiri, Bungu na kadhalika?

(b) Je, Serikali haioni kuwa ni vema matengenezo hayo yaende sambamba na ujenzi wa nyumba za watumishi (Mahakimu) katika maeneo hayo?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Eng. Laus Mhina Mbunge wa Korogwe Vijijini, lenye sehemu (a) na (b), napenda kumpongeza kwa dhati kwa jinsi anavyofuatilia kwa karibu sana maendeleo ya Mahakama hasa katika Wilaya ya Korogwe. Baada ya pongezi hizo sasa napenda kujibu swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inaona umuhimu wa kuyafanyia matengenezo makubwa au kujenga majengo mapya katika maeneo si, Magoma, Vugiri na Bungu tu bali katika Mikoa na Wilaya

zote nchini. Hata hivyo, juhudi za ujenzi wa majengo ya Mahakama zinakwamishwa na ufinyu wa bajeti inayotengwa kwa ajili hiyo. Hivi sasa Serikali inaendelea na ujenzi wa majengo ya Mahakama za Mwanzo pale Babati Mjini; Lugoba(Bagamoyo), Karabagaine (Bukoba) na Mugango (Musoma). Ujenzi wa Mahakama za Mwanzo za Maposeni na Lumbingu (Songea) umekamilika na taratibu za kuzipatia Mahakama hizo samani unaendelea.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa bajeti, Serikali haina mpango hivi sasa wa kuanzisha mradi mpya wa ujenzi au ukarabati hadi pale miradi inayoendelea itakapokamilika.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inaona ni vema na kwa kweli ni sera ya Serikali hivi sasa kwamba matengenezo na ujenzi wa majengo ya Mahakama uende sambamba na ujenzi wa makazi ya Mahakimu katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, hali ya Mahakama zetu nyingi si nzuri, naomba kupitia Bunge hili kutoa wito kwa uongozi wa Wilaya ya Korogwe na hasa Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe na Halmashauri zote nchini kutenga fedha na kuwahamasisha wananchi kujenga Mahakama za Mwanzo katika maeneo yao kama moja ya shughuli za maendeleo kwa kushirikiana na Mahakama ya Tanzania. (*Makofi*)

**MHE. ENG. LAUS O. MHINA:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na majibu mazuri ya Waziri hususan pale anaposema kwamba ni vema kwanza tukamilishe miradi inayoendelea kuliko kuanzisha miradi mipya. Kutokana na hali ilivyo katika Jimbo langu la Korogwe Vijijini, je, itawezekana kutoa kipaumbele mara miradi hii inayoendelea itakapokamilika? Tuanze sasa katika Jimbo la Korogwe Vijijini.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, napenda nimwahidi yeye na wananchi wa Korogwe kwamba baada ya kukamilisha miradi hii tunayojenga sasa zikiwemo Mahakama 20 ambazo tuliweka katika bajeti yetu ya mwaka huu, tutaipa kipaumbele Wilaya ya Korogwe na kwenda kuangalia uwezekano wa kukarabati ama kujenga upya Mahakama hizo tatu alizozitaja.(*Makofi*)

**MHE. DK. WILBROAD P.SLAA:** Mheshimiwa Spika nakushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa Waziri amekiri hali ya Mahakama nchi nzima ni mbaya na kwa kuwa Wilaya ya Karatu haina Mahakama ya Wilaya lakini kuna majengo ya Mahakama ya Mwanzo baada ya Serikali kukamilisha jengo jipya la Mahakama ya Mwanzo, je, Serikali sasa ipo tayari Mahakama ya zamani angalau kama haiwezekani kutumia Mahakama mpya kama Mahakama ya Wilaya angalau ile ya Mwanzo ambayo nayo ina hali bora zaidi kuliko hata Mahakama ya Monduli ambapo wananchi wa Karatu wanapelekwa sasa na wanateseka kwa ajili ya umbali na hakuna usafiri na Wizara ina taarifa hiyo?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, suala alilolileta mbele ya Bunge lako leo ni suala ambalo alikwishalileta kwenye ofisi yangu na leo hii pia amelileta tena kwa barua. Kwa kuzingatia umuhimu wa suala hilo tayari nimekwishaagiza leo hii, Wizarani iundwe timu ambayo itakwenda kutembelea Mahakama ya Mwanzo ya Karatu, Kasulu na Muhutwe kwenda kuangalia jinsi tunavyoweza kutatua tatizo hili hasa la Dokta Slaa. (*Makofi*)

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge majibu mazuri hayo yanatosheleza, sasa ni zamu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na swali linalofuata linaulizwa na Dk. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya.

Na. 142

**Kuongezeka kwa Idadi ya Watu WasiojuaKusoma na Kuandika**

**MHE. DK. CHRISANT M. MZINDAKAYA** aliuliza:-

Kwa kuwa elimu ya watu wazima inazidi kushuka na sasa idadi ya watu wasiojua kusoma na kuandika inaongezeka na kwa kuwa walimu wanaojitolea hulipwa Tshs. 20,000/= tu kwa mwezi; tena mara nyingi hawalipwi kwa wakati:-

Je, Serikali itachukua hatua gani kurekebisha hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU M. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dk. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, Mbunge wa Kwela kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ilitoa waraka wa elimu namba 3 mwaka 2006, kuzielekeza Halmashauri zote nchini kutenga fedha za kugharamia Elimu ya Watu wazima ikiwa ni pamoja na kulipa wawezeshaji Honoraria ya Shilingi 20,000/= kwa mwezeshaji.

Mheshimiwa Spika, kulingana na ufinyu wa bajeti Halmashauri nyingi hazitengi fedha za kutosha kulipa honoraria kwa wawezeshaji wote. Hali hii husababisha baadhi ya vituo vya kujifunzia kufungwa kutokana na walimu wa kujitolea kutolipwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na tatizo la kuongezeka kwa idadi ya watu wasiojua kusoma na kuandika, Serikali imekusudia kuendeleza Elimu ya Watu Wazima kwa kutekeleza Mpango wa Elimu ya Msingi kwa walioikosa MEMKWA na Mpango wa Uwiano kati ya Elimu ya Watu Wazima na Jamii MUKEJA na NDIYO NINAWEZA. MEMKWA hutoa fursa kwa watoto wa miaka 11-14 na vijana wa miaka 15-18 ambao walikosa elimu ya msingi katika mfumo rasmi. Utaratibu huu una lengo la kupunguza idadi ya watu wazima wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu. MUKEJA hutoa fursa kwa watu wazima wa miaka 19 na zaidi kujua kusoma, kuandika na kuhesabu pia huwaongezea ujuzi na uwezo wa kuendesha kwa ufanisi shughuli zao mbalimbali za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Cuba inatekeleza mpango wa Maendeleo ya Kisomo wa NDIYO NINAWEZA, utakaotekelezwa kwa njia ya redio na video. Aidha, mpango huu utajikita katika stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu pamoja na maarifa

yanayohusiana na maisha ya kila siku. Wizara iko katika hatua ya mwisho ya kutoa mafunzo kwa wawezeshaji wa mpango huu.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa MEMKWA, MUKEJA, na NDIYO NINAWEZA utaongeza idadi ya watu wanaojua kusoma, kuandika, na kuhesabu. Mipango hii pia itasaidia juhudi za kuondoa umaskini, kufuta ujinga na kujenga mwelekeo sahihi kwa wananchi kuendelea kujielimisha katika maisha yao.

**MHE. DK. CHRISANT M. MAJIYATANGA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa swali langu la msingi lilihusu kuondoa tatizo la kutokuwalipa Walimu wanaojitolea na Waziri amejibu kwamba walishatoa waraka. Kwanza, je, kuna faida gani ya kutoa waraka usioweza kutekelezwa? Pili, Waziri anaweza akatoa takwimu sasa za kushuka kwa elimu ukilinganisha na mafanikio ya nyuma, sasa tumeshuka kwa kiwango gani kwa elimu ya watu wazima?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU M. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, kutokana na kugatua madaraka na kupeleka masuala kadhaa kwa Serikali za Mitaa chini ya Wakurugenzi wa Halmashauri, si rahisi kwa Wizara ya Elimu kuweza kubakia na kipengele hicho cha kulipa honoraria, ndiyo maana waraka ulitolewa na ukapelekwa kwenye Halmashauri chini ya kifungu au Vote Na. 5 ambako ndiko kwenye kasma ya elimu ya watu wazima. Kwa hiyo, naomba tu kutoa wito kwamba Wakurugenzi wote nchini na hasa kwa vile sasa tupo kwenye mchakato wa bajeti wa mwaka 2010/2011, basi wazingatie kuweka hizo honoraria na wawapatie.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kabisa kwamba kiwango cha wasiojua kusoma na kuandika kimeongezeka na inahisiwa asilimia 30 ya Watanzania hivi sasa hawajui kusoma na kuandika.

**MHE. SUZAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa, swali la msingi linahusu idadi ya watu wasiojua kusoma na kuandika kuongezeka na kwa kuwa suala hili linatokana na sababu mbalimbali ikiwemo pia wahitimu wa darasa la saba baadhi yao wanahitimu bila ya kujua kusoma na kuandika. Je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha kwamba wahitimu wa darasa la saba wanamaliza wakijua kusoma na kuandika?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI MHE. MWANTUMU M. MAHIZA:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ambayo ndiyo yenye dhamana ya elimu kwa nchi hii, imeweka mikakati kadhaa ambayo muda si mrefu Serikali au Wizara itatoa waraka.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba imebainika baadhi ya wanafunzi hawajui kuandika wala kusoma, taarifa ya mkakati huo ni kubwa na kwa kuwa Mheshimiwa Suzan ni mmoja wa wanakamati wa huduma za jamii, naomba taarifa ile tupitishe kwenye Kamati kwanza kabla ya kuitoa kwa Taifa zima. Ahsante.

Na. 143

**Ujenzi wa Shule za Sekondari kila Kata Nchini**

**MHE. PAUL P. KIMITI** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika zoezi la ujenzi wa shule za sekondari kwa kila Kata hapa nchini, maeneo ya Mijini yamekuwa na matatizo ya kutopata ardhi ya kutosha kwa ajili ya shule hizo na hivyo kuhitaji majengo ya shule za Mijini yawe ya ghorofa:-

(a) Je, kwa nini fedha zinazotolewa kwa shule za Mijini zisizingatie ukweli huo?

(b) Je, isingekuwa vema kwa mabweni na maabara katika shule hizo kupewa umuhimu kwanza ili kuimarisha ubora wa elimu na nidhanu hasa kwa wasichana watakaoishi katika mabweni.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU M. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paul Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, fedha zinazotolewa kwa ajili ya ujenzi wa shule za Sekondari zikiwemo za Mijini ni ruzuku inayotolewa ili kuunga mkono nguvu na jitihada za wananchi katika ujenzi wa shule za sekondari kwa kila Kata hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Serikali inashauri Halmashauri na wananchi walio kwenye maeneo yenye uhaba wa ardhi kuongeza nguvu zaidi ili kujenga shule za sekondari za maghorofa.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa maabara katika shule za Sekondari nchini ndiyo maana kipaumbele cha kwanza katika mwaka 2010-2015 ni ujenzi wa maabara.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa mradi mkubwa wa kujenga na kufunga vifaa vya maabara katika shule zote za sekondari za Serikali hapa nchini. Gharama za mradi wote inakadiriwa kuwa dola za Kimarekani 562 milioni. Serikali inajadiliana na wahisani mbalimbali wa maendeleo wakiwemo Benki ya Dunia kupitia awamu ya pili ya mpango wa MMES ili kupata fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, kimsingi shule za sekondari za Kata ni za kutwa. Hata hivyo pale ambako upo mtawanyiko wa makazi katika Kata au shule kuwa mbali na makazi tunawaomba wananchi washirikiane na uongozi wa Kata kujenga hosteli na kuziendesha.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza kabisa nataka nitumie nafasi hii kumpongeza msichana anayeitwa Emmaculata Mosha kwa kazi nzuri aliyoifanya kuwa msichana wa kwanza

na hii ni dalili ya kwamba matumizi ya bweni imesaidia sana wasichana waweze kufanya vizuri zaidi katika masomo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba ujenzi wa Maabara katika mwaka huu wa fedha tungeomba uende sambamba na ujenzi wa mabweni kwa wasichana ili kupunguza kasi ya watu wanaoitwa mafataki jina ambalo mimi ningeomba liangaliwe upya kwa sababu Fataki ni jina la Babu yangu nisingependa liendelee kutumika kama sehemu ya jina watafute jina jingine. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, nchi yeyote duniani hutunga sheria na taratibu kuzingatia mazingira ya mahali penyewe, na ndiyo maana katika Vita Kuu ya Pili Waingereza waliruhusu Singasinga wapigane vita bila kuvaa helmeti wakaendelee na vilemba vyao, je, Waziri atakubaliana nami kwamba mpango tulioomba sisi Waheshimiwa Wabunge kwamba fedha zinazotolewa kwa kila Kata zitegemee na umbali wa mahali penyewe na gharama za mahali penyewe, kuliko kutoa fedha sawa kwa wote, watu wa Dar es Salaam, Sumbawanga, Ngara, Tunduru na kadhalika? Je Serikali itaangalia upya utaratibu wa fedha hizo?

**SPIKA**: Ahsante sana, bahati mbaya Mheshimiwa Paul Kimiti hakutueleza kama huyu Babu yake anayeitwa Fataki kweli hakuwa Fataki. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU M. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nimpongeze na nimshukuru sana kwa kutuunga mkono katika vita ya kupambana na Mafataki, tutawatafutia jina lao baada ya kikao hiki.

Mheshimiwa Spika, tunakubaliana kabisa na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge kwamba ujenzi wa maabara uende sambamba na mabweni, tunaamini, tunatambua na tunafahamu kwamba kupatikana kwa mabweni ni kuongeza ustawi utulivu na umakini kwa wanafunzi wakati wanapojifunza, naomba niseme kwamba kwa niaba ya Waziri wa TAMISEMI tumelipokea na tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari fedha zake huwa zinatolewa kwa uwiano, kwa sababu awali zilikuwa zinagawiwa kutegemea na mazingira, tukaona kuna matatizo mengi, lakini kwa kuwa mpango huu hivi sasa upo chini ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, naomba niseme tu kwa pamoja tutashirikiana ili kuona kwamba fedha zinazopelekwa zinakwenda kwa kutegemea na hali na mazingira yalivyo. Tunaupokea ushauri. (*Makofi*)

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa matatizo ya ukosefu wa ardhi mijini kwa kiasi kikubwa sana kunachangiwa na utendaji mbovu wa Halmashauri ambazo kisheria zimepewa mamlaka za kugawa ardhi ambazo ziko katika maeneo yao, kama ambavyo tumeshuhudia katika Manispaa ya Kinondoni. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri haoni kwamba kuna umuhimu wa Wizara hizi tatu kuweza kufanya kazi kwa karibu nikimaanisha Wizara ya TAMISEMI, Wizara ya Ardhi na Wizara ya Elimu ili kuhakikisha kwamba maeneo yote ya shule yanakuwa na viwanja muhimu kwa ajili ya watoto ambao pamoja na mambo mengine itasaidia ujenzi wa shule?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU M. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mdee, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo. Ushauri wake ni mzuri na kwa kuwa Mawaziri wote watatu wako hapa wamemsikia na kwa hakika wataketi pamoja ili kuweza kuweka vipaumbele katika masuala ya ardhi kwa ujenzi wa shule. Ahsante.

Na. 144

**Tatizo la Maji-Jijini Dar es Salaam**

**MHE. CHARLES N. KEENJA** aliuliza:-

Kwa kuwa upatikanaji wa maji katika Jiji la Dar es Salaam ni asilimia 56 tu na kwa kuwa upatikanaji wa maji katika maeneo ya pembezoni kama vile Kibwegere, Mpiji, Magohe, Msumi, Kwembe ni asilimia sifuri licha ya kuwepo kwa mtandao mzuri wa mabomba ya kusambaza maji yasiyokuwepo:-

(a) Je, kuna mipango gani ya kuondoa matatizo ya maji kwenye Jiji la Dar es Salaam na itachukua muda gani kuitekeleza?

(b) Je, mipango hiyo itagharamiwaje?

(c) Kwa kuwa miradi ya maji ya Goba na Msewe inalipiwa na wananchi kwa gharama kubwa zaidi ya mara tano ya wale wanaohudumiwa na *DAWASCO*; je, ni lini Serikali itaichukua miradi hiyo na kuwaondolea wananchi mzigo mkubwa wa kulipia maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Charles Ndelianaruwe Keenja, Mbunge wa Ubungo, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, katika jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo, eneo linalohudumiwa na *DAWASA/DAWASCO*, kiwango cha utoaji wa huduma ya maji safi na salama kimefikia takribani asilimia 68 na maji yanapatikana kwa wastani wa saa nane kwa siku. Kiwango hiki bado hakiridhishi kutokana na kukua kwa kasi kubwa ya jiji hilo ambapo idadi ya watu inakadiriwa kuongezeka kwa wastani wa asilimia nane kwa mwaka tofauti na wastani wa Kitaifa wa kukua kwa miji ambao ni asilimia 4.6.

Mhesihmiwa Spika, baada ya maelezo haya, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kuongeza upatikanaji wa maji, Wizara yangu, kupitia *DAWASA* kati ya mwaka 2003 na 2009 ilitekeleza mradi wa kukarabati mfumo wa usambazaji maji kwa kuweka mtandao wa mabomba yenye urefu wa kilometa 1132.5,

kukarabati mitambo mitatu ya kuchuja maji ya Mtoni, Ruvu Juu na Ruvu Chini, kujenga magati 490 ya kuchotea maji na kuwafungia mita wateja 65,000. Aidha, mfumo wa umeme unaotumika kuendesha mitambo ya maji uliboreshwa kwa kufunga *transforma* nne mpya, mbili katika kituo cha Ruvu Juu na mbili katika kituo cha Ruvu Chini.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza wingi wa maji, Serikali imeanza kutekeleza mradi wa kupanua kituo cha maji cha Ruvu Chini, uchimbaji wa visima virefu 12 huko Kimbiji na vinane (8) huko Mpera.

Miradi mingine iliyoandaliwa ni ujenzi wa bwawa la Kidunda na mradi wa kupunguza upotevu wa maji katika baadhi ya maeneo wakati mtandao mpya kabisa utawekwa katika maeneo sugu ya Tegeta-Bunju, Bunju-Bagamoyo na Mbezi Mwisho-Kiluvya.

(b) Mheshimiwa Spika, miradi yote itagharamiwa na Serikali ya Tanzania kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Maji *(WSDP)* ambayo itashirikiana na Serikali ya Marekani kupitia Shirika la *Millenium Challenge Corporation (MCC)* kwa kutekeleza miradi ya kupanua kituo cha Ruvu Chini, ujenzi wa bwawa la Kidunda na mradi wa kupunguza upotevu wa maji. Aidha, Serikali ya Norway itashiriki kugharamia mradi wa uchimbaji wa visima 20 nilivyovitaja.

(c) Ni kweli kwamba wananchi wa Goba wanahudumiwa na Umoja wa Watumia Maji wa Goba *(Goba Water Users Association)* kwa gharama kubwa zaidi ya ile wanayolipa wateja wanaohudumiwa na *DAWASCO*.

Bei kubwa inayopangwa na Umoja huo wa watumia maji inasababishwa na gharama za kusukuma maji *(pumping cost)* kwenda katika maeneo ya mwinuko pamoja na gharama za uendeshaji wa Umoja huo. Kwa kuwa Wizara yangu sasa imeanza kutekeleza mradi wa kuweka mtandao wa usambazaji wa maji katika eneo la Goba, wananchi wengi wataunganishwa kwenye mtandao huo, hivyo kuwapunguzia gharama za maji.

Mheshimiwa Spika, njia nyingine ninayoiyona ni kufanya mazungumzo kati ya Umoja wa Watumia Maji na Halmashauri ya Manispaa inayohusika ili kutafuta uwezekano wa Halmashauri kutoa ruzuku katika gharama ya uendeshaji mpaka hapo mtandao mpya wa bomba utakapokamilika.

**MHE.CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu niulize maswali madogo ya nyongeza na nianze kwa kuishukuru na kuipongeza Wizara kwa ujenzi wa mtambo wa maji katika jiji la Dar es Salaam na kuboresha vianzio vya maji. Kwa kuwa mpango wa kupata maji kutoka Kimbiji na Mpewa unaelekea kuwa wa uhakika zaidi kuliko mipango mingine yote, je, Serikali inachukua hatua gani sasa kuchimba visima ishirini vinavyohitajika na kujenga mfumo wa kuchukua hayo maji kutoka kwenye visima hivyo kupeleka kwenye maeneo yanayohusika?

Mashule mengi ya Dar es Salaam yana watoto wengi sana, elfu mbili, wengine hata elfu tatu na kuendelea. Bila maji watoto wale wanaishi katika mazingira magumu sana. Je Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kwamba shule hizi zinapata maji ili kulinda usafi na afya hususan kwa wasichana?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI**: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Keenja kama ifuatavyo: Ni kweli kabisa sasa tumeanza utekelezaji wa kuchimba maji chini ya ardhi maeneo ya Kimbiji na Mpera na hatua tuliyofikia sasa ni nzuri kwa sababu tayari tumeanza mchakato wa kupata mkandarasi wa kuchimba visima hivyo. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Keenja awe na subira kidogo kwa sababu ndani ya miezi minne tu ataanza kuona kazi hii ya uchimbaji wa visima katika eneo hilo la Kimbiji na Mpera, kwa kweli tumedhamiria kufanya kazi hiyo kwa sababu inaelekea kuwa na uhakika zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la shule za sekondari na shule za msingi katika Jiji la Dar es Salaam, niseme tu kwamba mipango yote hii ya kuongeza maji, upatikanaji wa maji katika Jiji inawahusisha wananchi wote, wananchi wa kawaida, mashule na taasisi mbalimbali. Lakini kwa upande wa shule labda ningependa kusema kwamba uzoefu nilioupata juzi nilipokuwa katika Mikoa ya Lindi na Mtwara wa kuchimba matanki kidogo kwa ajili ya kuvuna maji kwa kutumia paa za nyumba umesaidia sana shule za sekondari katika Mikoa ile ya Lindi na Mtwara na gharama yake ni ndogo, yawezekana katika Dar es Salaam ikawa ardhi ni haba lakini pale inapowezekana basi ni vizuri tuanze kutumia hata utaratibu wa kuvuna maji kwenye paa za nyumba kwa ajili ya wanafunzi wetu.

**SPIKA:**Waheshimiwa muda wa maswali umepita, maswali yamekwisha, sasa ni matangazo kama ifuatavyo.

Nikianza kama kawaida na wageni. Tunao wageni saba wa Mheshimiwa Dk. Batilda Buriani, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira wakiongozwa na Bi. Ruth Mollel, Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais. Huyu ni mmoja wa akina mama Makatibu Wakuu wenye uzoefu mzuri na tunaupongeza utumishi wako Ruth, naomba na wengine wasimame hawakutajwa hapa lakini nadhani ni Wakuu wa Idara katika Ofisi ya Makamu wa Rais. Ahsanteni sana.

Tunao wageni kutoka Mufindi wa Mheshimiwa Joseph Mungai na Mheshimiwa Benito Malangalila, Mufindi Kasikazini na Kusini ambao ni Madiwani arobaini wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mufindi, Ndugu Naused Nyagamilwa, naomba asimame peke yake kwanza. Ndiyo Mwenyekiti ya Halmashauri ya Mufindi, pia yupo Mheshimiwa Yohanes Kaguo, Makamu Mwenyekiti ambae pia ni Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Mufindi. Lakini pia miongoni mwao wapo Katibu Mwenezi wa CCM ambae ni ndugu Daudi Yasin, huyu Daudi maarufu sana ni Msimamizi na Mratibu wa Kombe la Muungano linalochezwa kila mwaka, hongera sana ndugu Yasin.

Pia wapo Maafisa Waandamizi wa Halmashauri ndugu Lupembe na ndugu Mwakilema, sijui nimelipatia hilo jina, basi Waheshimiwa Madiwani wa Mufindi sasa msimame ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuwaona. Inaonekana hii Wilaya ya Mufindi ina neema maana yake Madiwani wote wamenawiri vizuri tu, ahsanteni sana na mtusalimie huko mkirudi.

Pia tuna wageni wa Wabunge wa Mkoa wa Rukwa ambao ni wanafunzi kumi waliopo *UDOM* kutoka Mkoa wa Rukwa wanaongozwa na ndugu Cletus Mwanauta. Wale wanafunzi

kumi kutoka Mkoa wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana, tunawatakia mema katika mafunzo yenu, nchi inawahitaji sana mfanye kazi kwa bidii.

Wapo wageni wa Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo: Ndugu Aidan Majawanga, halafu na ndugu Shabani Mtego hawa wawili wamehama chama kutoka *TLP* ndugu Aidan Majawanga alikuwa ndiyo Katibu wa Mkoa wa *TLP* Kilimanjaro.

Ndugu Shaban Mtego ambae ni hodari sana kwa kuongea jukwani, huyu ni Mwenezi *TLP* Mkoa, ambaye amehamia CCM kwa juhudi za Mheshimiwa Aloyce Kimaro. Pamoja nao yupo Ndugu Festo Moshi ambaye hakutajwa, sasa ni nani lakini nadhani ni mmoja wa wana CCM kule Vunjo, ahsante sana. Karibuni sana kutoka Vunjo. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Shally Raymond ambao ni Godliving Moshi, Mwenyekiti wa UVCCM Kilimajaro na ndugu Mercy Mollel, Katibu wa UVCCM Moshi vijijini, karibuni sana.

Pia tuna mgeni wa Mheshimiwa Benson Mpesya ambaye ni ndugu Teddy, karibu sana. Tunao leo wageni kutoka gazeti la Mwananchi ambao ni Daniel Mwaijega, Mhariri wa mwananchi Jumapili, leo wamekuja rasmi sio kuandika mambo, leo wamekuja tu kushuhudia Bunge na ndugu Rashid Kejo, Mhariri wa makala ya Mwananchi, nalipenda kulisoma gazeti hili lakini lah, mara nyingine basi ndiyo hivyo hivyo. CCM inasimamia demokrasi, kwa hiyo hata kupanua haya mambo wengine wanasema hivi, ukisema hivi nayo ni sehemu tu ya uhuru wa wananchi.

Vile vile wapo wanafunzi kumi na mbili wa mwaka wa pili kutoka St. John’s *University* wanaosoma masomo ya Sayansi ya Ualimu wale wanafunzi kumi na mbili wa St. John’s tafadhali, wanaongozwa na ndugu Ephraim Kalumanga, karibuni sana nanyi pia tunawatakia mafanikio katika masomo yenu.

Huo ndio mwisho wa orodha ya wageni wetu, naomba kutangaza kwamba hapa Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Mohamed Missanga anasema kwamba leo saa tano asubuhi mara baada ya maswali Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu mkutane katika ukumbi wa Msekwa B, kikao muhimu sana hiki kinazingatia taarifa muhimu sana, wote muwepo bila kukosa.

Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama naye pia anaomba wajumbe wote wa Kamati hiyo mkutane hapo saa tano katika ukumbi namba 231, huu ni Muswada muhimu sana ulio mbele yetu na ili kuzisukuma kazi za Bunge ziendelee nasihi sana wajumbe wote wa Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama saa tano asubuhi hii, basi wakutane katika ukumbi namba 231.

Mheshimiwa Omar Kwaangw’, Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii anaomba leo saa saba mchana Wajumbe wa Kamati hiyo mkutane katika ukumbi mpya wa sherehe namba 105 *basement* hapa hapa, chini ya jengo hili.

Vile vile Mheshimiwa William Shelukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini anatoa mwito kwa wajumbe wote wa Kamati hiyo ya Nishati na Madini, mkutane leo saa saba ukumbi namba 219, ghorofa ya pili jengo la Utawala.

Pia Mheshimiwa John Momose Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali, anawaomba wajumbe wote wa Kamati hiyo wakutane leo tarehe 9 Februari kuanzia saa saba katika ukumbi wa tafrija moja ya ukumbi mpya.

Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala anahitaji na nimeidhinisha hivyo, Wajumbe wote wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kuzingatia Muswada muhimu wakutane saa tano asubuhi hii katika ukumbi mkubwa ule wa Pius Msekwa.

Pamoja na yote hayo, nimeitisha kikao cha dharura cha Kamati ya Uongozi saa tano kamili, ningeomba pale ambapo Mwenyekiti wa Kamati anaendesha kikao basi Makamu wa Mwenyekiti awepo yaani mmoja wao awepo kwenye Kamati ya Uongozi saa tano asubuhi hii katika Ukumbi wa Spika.

Hayo ndiyo matangazo ya leo na kwa kuendeleza shughuli na kuniwezesha kuongoza kikao cha Kamati ya Uongozi, namwita sasa Mheshimiwa Zuberi Ali Maulid, Mwenyekiti ili aendelee na shughuli zilizosalia. Ahsante.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Zuberi Ali Maulid) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea.

## HOJA ZA KAMATI

### Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira Kuhusu Athari za Mazingira za Mgodi wa Dhahabu Barrick - North Mara

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu athari za mazingira katika mgodi wa North Mara. Mwenyekiti au mwakilishi wake, namwona Prof. Mwalyosi atakuja kuwakilisha kwa niaba ya Mwenyekiti.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI (k.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu ya Kanuni ya 115 ya Kanuni za Bunge toleo la 2007, naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwakilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu athari za mazingira na za kijamii katika mgodi wa dhahabu wa North Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari hizi ziliripotiwa kwanza na vyombo vya habari na baadaye na Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira katika Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge la Bajeti na ilipendekeza Kamati Maalum iundwe ili kufuatilia suala hilo. Athari hizo, zilihusu uvujaji wa kemikali za sumu kutoka mgodi wa dhahabu wa North Mara, Wilaya ya Tarime, Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufuatiliaji wa athari za mazingira. Serikali iliunda Kamati Maalum iliyohusisha Mawaziri kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, Wizara ya Nishati na Madini na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na baadhi ya wajumbe kutoka Kamati za Kudumu za Bunge za Ardhi, Maliasili, Mazingira na Nishati na Madini. Kamati Maalum ilifanya ukaguzi katika eneo la mgodi na kutoa taarifa mbili kwa Spika, moja ya Serikali (Kiambatisho Na. 1) na nyingine ya Bunge (Kiambatisho Na.2). Baada ya kutafakari, Mheshimiwa Spika aliunda Kamati ndogo iliyojumuisha wajumbe kutoka Kamati za Kudumu za Bunge za Ardhi, Maliasili na Mazingira na Nishati na Madini ili kuchambua ripoti hizo kwa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ndogo ilikubaliana na yalioainishwa na Kamati Maalum kuhusu mgodi wa North Mara (Kiambatisho Na.2), pamoja na mambo mengine Kamati hiyo ndogo ilipendekeza mgodi ufungwe kwa muda ili kuwezesha marekebisho yaliyopendekezwa yafanyike (Kiambatisho Na. 3). Mapendekezo hayo yalijadiliwa na Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira na Serikali. Serikali ikapendekeza kupewa fursa ya kufanya marekebisho ya mapungufu yaliyojitokeza katika mgodi huo badala ya kuufunga mgodi kwa muda. Kamati pamoja na kukubaliana na Serikali, iliamua kujiridhisha kwa Kamati nzima kutembelea mgodi wa *North Mara* tarehe 21/10/2009 ili kubaini kwa makini zaidi mapungufu ya mgodi na kuipa Serikali maagizo mahsusi. Katika ziara ile Kamati ilipitia migodi ya dhahabu ya Buzwagi na Geita kabla ya kuelekea mgodi wa dhahabu wa *North Mara.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaliyojitokeza Katika Ziara. Ili kujua hali ya mazingira ya mgodi kwa wakati huo, Kamati ilifanya mazungumzo na uongozi wa Mkoa, Wilaya, Barrick-North Mara na wananchi. Matatizo yafuatayo yalijitokeza:-

(i) Madai ya uvujaji wa Kemikali za sumu kutoka mgodini ulioleta athari katika mazingira yanayozunguka mgodi.

(ii) Madai ya uchafuzi wa vyanzo vya maji vya wananchi ikiwa ni pamoja na mto Tigithe, visima vya maji na maeneo oevu.

(iii) Madai ya kuwepo kwa udhaifu kwa upande wa Serikali na mgodi katika kushughulikia afya za wananchi walioathirika na uvujaji wa sumu kutoka mgodini.

(iv) Mahusiano mabaya baina ya Uongozi wa mgodi na wanachi kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo wananchi waliotakiwa kuhama kulipwa fidia ndogo isiyoridhisha na kukosekana kwa ajira kwa wananchi wa vijiji vinavyouzunguka mgodi.

(v) Kiwango kidogo cha mrahaba (*Royalty*) kinachotolewa na mwekezaji kwa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime (kiasi cha dola laki mbili kwa mwaka ambacho ni chini ya thamani ya kinoo kimoja cha dhahabu ukilinganisha na wastani wa mapato ya mwekezaji anayoyapata).

Mheshimiwa Spika, Maagizo ya Kamati na utekelezaji wake kati ya Novemba - Desemba 2009. Nasisitiza, ni maagizo ya Kamati na Utekelezaji wake kati ya Novemba na Desemba 2009 na sio nje ya utaratibu huo. Kufuatia ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge katika mgodi wa dhahabu wa North Mara, Kamati ilitoa maelekezo mahsusi kwa Serikali na kutekelezwa kama ifuatavyo:-

- Agizo Na. 1. Kufanya utafiti wa kina na kutoa taarifa za kitaalam kuhusu watu wote walioathirika na vifo vyote vya binadamu na mifugo vilivyojitokeza.

Utekelezaji: Lengo ni kuthibitisha pasipo mashaka yoyote kuwa binadamu na mifugo walioathirika kutokana na kemikali zilizovuja kutoka mgodini na si vinginevyo. Agizo hili halijatekelezwa. Serikali imeeleza hii ni kutokana na uhaba wa fedha kwa kipindi hiki. Serikali imeahidi kutekeleza agizo hili baada ya Bajeti ya mwaka ujao wa Fedha 2010/2011.

- Agizo Na. 2. Kutoa maelekezo ya kina na yenye ratiba ya utekelezaji kwa mwekezaji kuhusu urekebishaji wa kasoro za mazingira zilizojitokeza.

Utekelezaji: Maelekezo ya kina na yenye muda wa utekelezaji kwa mgodi yalitolewa na *NEMC* na yamefanyiwa kazi kama vile, kuondosha lundo la mawe taka yenye kuzalisha tindikali; mabwawa ya kutunzia maji yenye tindikali kuwekewa majamvi, kujengewa uzio na kuimarishiwa ulinzi; kuchimbwa kwa mitaro ya kukusanya maji taka yanayovuja na kuyarejesha kwenye mabwawa ya hifadhi na pia kuandaa mpango wa kudumu wa kurekebisha uvujaji huo. (Kiambatanisho Na. 4)

- Agizo Na. 3. Serikali ifuatilie suala la ujirani mwema baina ya mgodi na wananchi wanaouzunguka mgodi ili kuboresha uhusiano kati ya Kampuni na wananchi.

Utekelezaji: Agizo hili linatekelezwa kwa kiasi cha kuridhisha. Serikali imepanga kufanya utafiti wa kina kuhusu masuala ya kiuchumi na kijamii na pia inafanya mchakato wa kumpata Mtalaam Mwelekezi wa kufanya utafiti huo unaohusu mahitaji ya kiuchumi na ya kijamii.

Kwa upande mwingine, Serikali imeunda Kikosi Kazi kwa kila kijiji ili kupitia mikataba yote na kubaini upungufu unaojitokeza ili kuhakikisha makubaliano yaliyowekwa na Kampuni yanafanyika. Vile vile Vikosi Kazi hivyo, vitafuatilia namna gani wananchi wanafaidika na mgodi kama vile kupata fidia stahiki, ajira na kuwezesha katika miradi mbalimbali.

Aidha, mwekezaji vile vile ameajiri Afisa Uhusiano atakayekuwa kiunganishi kati ya mgodi na wananchi katika masuala ya kiuchumi na ya kijamii.

- Agizo Na. 4. Serikali itafute ufumbuzi wa haraka kuhusu upatikanaji wa vyanzo vya maji mbadala.

Utekelezaji: Maandalizi ya awali kutekeleza agizo hili yamefanyika ambapo Serikali inashughulikia suala la kutafuta vyanzo vya maji mbadala. Utambuzi wa vyanzo vya maji tayari umefanyika katika vijiji tisa. Serikali inakadiria kutumia kiasi cha shilingi milioni 250 kwa miradi hiyo na mwekezaji anashauriwa kushiriki katika kugharamia sehemu ya gharama ya miradi hiyo.

- Agizo Na. 5, fidia kwa wananchi waliobaki katika eneo la mgodi likamilishwe.

Utekelezaji: Hadi sasa haujakamilika kwani zoezi la mazungumzo na maridhiano kati ya wananchi wenye ardhi na makazi kwa upande mmoja na kampuni kwa upande mwingine bado linaendelea.

- Agizo Na. 6: Serikali iangalie upya suala la utoaji leseni kwa watu wanaozunguka eneo la mgodi ili kuondoa tofauti na matatizo yanayojitokeza ya wachimbaji wadogo kuingia kwenye eneo la mgodi.

Utekelezaji: Utoaji wa leseni upo atika hatua za awali ambapo maeneo ya uchimbaji mdogo nje ya eneo la mgodi, yametambuliwa. Timu ya Watalaam imeundwa kwa ajili ya kupanga tathmini na kupima maeneo husika. Aidha, maeneo ya wachimbaji wadogo kutoka ndani ya eneo la mgodi yamependekezwa na kuwasilishwa kwa Wizara ya Nishati na Madini kwa maamuzi mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa, Kamati inatoa ushauri kwa kila agizo kama ifuatavyo:-

Agizo la kwanza, ikumbukwe kwamba agizo la kwanza ilikuwa ni kufanya utafiti wa kina na kutoa taarifa za kitaalam kuhusu watu wote walioathirika na vifo vyote vya binadamu na mifugo vilivyojitokeza. Kwa hiyo, Kamati imeagiza, kwa kuwa suala hili linahusisha afya za binadamu na mifugo na hivyo kuwa la dharura, Serikali itafute fedha kwa haraka na kumshirikisha Mwekezaji. Lakini pili, tumesema, umakini utumike sana katika kuzingatia utafiti ambao utaonyesha uhakika wa uhusiano kati ya madhara kwa binadamu na mifugo na mimea na uchafuzi wa mazingira kutoka kwa binadamu, mifugo na mimea na uchafuzi wa mazingira kutoka mgodini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, agizo la pili, linahusu kutoa maelekezo ya kina na yenye ratiba ya utekelezaji kwa mwekezaji kuhusu urekebishaji wa kasoro za mazingira zilizojitokeza. Tunaagiza kwamba, Serikali ihakikishe inafuatilia maagizo yote yaliyotolewa yanatekelezwa kwa muda uliopangwa na watakaoshindwa kutekeleza, wawajibishwe. Vile vile tumeagiza taarifa zote kuhusiana na utekelezaji wa maagizo husika ziwasilishwe kwenye Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeagiza kuwa kutokana na kuwa mwekezaji ameshawasilisha mapendekezo ya hatua za kuchukua za kudumu katika Wizara ya Nishati na Madini tarehe 14 Januari, 2010, Kamati inaishauri, Wizara ichukue hatua za haraka ili yale yaliyopendekezwa na ambayo yanafaa yafanyiwe kazi mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, agizo namba tatu, lilisema Serikali ifuatilie suala la ujirani mwema baina ya mgodi na wananchi wanaozunguka mgodi ili kuboresha uhusiano kati ya kampuni na wananchi. Kamati inashauri, utafiti unaohusisha mambo ya kiuchumi na ya kijamii upangiwe muda maalum wa kukamilishwa isiachwe wazi. Lakini namba mbili haki za msingi za wananchi hususan afya na usalama wao, zizingatiwe katika utafiti huo. Aidha, wachimbaji wadogo wapatiwe maeneo ya kuendesha shughuli za uchimbaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, agizo la nne, lilihusu Serikali kutafuta ufumbuzi wa haraka kuhusu upatikanaji wa vyanzo vya maji mbadala. Kwa hiyo, tunaagiza kwamba, Serikali isimamie na kuhakikisha kwa kushirikiana na mwekezaji inagharamia upatikanaji wa maji safi na salama kwa haraka. Lakini naomba Serikali itoe muda maalum wa kukamilisha miradi hii ikizingatia umuhimu wa maji kwa jamii na kwa kuwa miamba ya asili inayozunguka mgodi ina asili ya kuzalisha kemikali na tindikali za sumu, *potential acid forming rocks*, ipo haja kwa miradi ya maji iliyoainishwa kufanyiwa tathmini ya athari ya mazingira yaani TAM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, agizo la tano, ni suala la fidia kwa wananchi waliobaki katika eneo la mgodi likamishwe. Kamati inashauri Serikali kuweka bayana utaratibu wa kuwatambua wanaostahili fidia hizo na kusimamia zoezi hilo kwa karibu zaidi ili wananchi wapate fidia stahiki na mbili kazi ya utambuzi iharakishwe ili waathirika walipwe kwa muda usiozidi miezi sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, agizo la sita, lilikuwa linasema Serikali iangalie upya suala la utoaji wa leseni kwa watu wanaozunguka eneo la mgodi ili kuondoa tofauti na matatizo yanayojitokeza ya wachimbaji wadogo kuingia kwenye eneo la mgodi. Tumesema mchakato wa kupata maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo uharakishwe na tathmini ya athari kwa mazingira yaani TAM ya maeneo haya igharamiwe na Serikali. Kwa sababu wananchi hawatakuwa na uwezo wa kugharamia tathmini hiyo basi Serikali igharamie kwa niaba yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya ziada. Hayo yalikuwa ni mapendekezo yaliyotokana na maagizo mahsusi yaliyotolewa na Kamati kwa Serikali lakini kuna mapendekezo ya ziada.

Moja, Serikali imeonyesha uwezo mdogo wa kufuatilia hali ya mazingira mgodini na kutegemea zaidi ripoti za mwekezaji. Kamati inashauri, Serikali iziwezeshe taasisi zake husika ili ziweze kutimiza wajibu wake.

Pili, maeneo oevu na bioanuai yaliathirika kwa kiwango kikubwa kutokana na utiririshwaji wa maji yenye kemikali za sumu kinyume na mahitaji ya Mkataba wa Kimataifa ya Hifadhi ya Bioanuai ambayo Serikali ya Tanzania imeridhia. Serikali izingatie kikamilifu masuala ya bioanuai wakati wa kutekeleza maagizo yanayohusiana na mgodi wa North Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, imeridhishwa na marekebisho yaliyofanyika hadi sasa katika miezi ile miwili Novemba-Desemba kuhusu uvujaji wa kemikali za sumu katika mgodi wa dhahabu wa North Mara. Hatua mbalimbali za kudhibiti hali hii zimechukuliwa na Serikali, mwekezaji na wananchi kwa kiwango cha kuridhisha. Vile vile hatua za ziada za udhibiti zinaendelea na nyingine zimependekezwa na Kamati. Kamati hii

inaamini kwamba, utimilivu wa juhudi hizi utarekebisha kwa ukamilifu matatizo yaliyojitokeza kwenye mgodi wa North Mara na hivyo kuondoa kabisa hoja ya kuufunga mgodi huo. Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuwa makini zaidi katika shughuli za migodi ya dhahabu siyo huo tu na mingine hususan zinazogusa maisha ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda kutoa shukrani za pekee, kwa Mheshimiwa Mbunge wa Tarime, Mheshimiwa Charles Mwera, kwa ushirikiano mkubwa alioipa Kamati hii katika kushughulikia suala hili la athari za mazingira za mgodi wa dhahabu wa North Mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vile vile niushukuru uongozi wa Mkoa, Wilaya na wananchi wa North Mara, kwa kushirikiana na Kamati hii kikamilifu wakati wa ziara ya Kamati katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninapenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, walioandaa Taarifa hii nao ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mwenyekiti na Mheshimiwa Hassan A. Khatib, Makamu wa Mwenyekiti. *(Makofi)*

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Arch. Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa James D. Lembeli, Mheshimiwa William Lukuvi, Mheshimiwa Zakhia H. Meghji, Mheshimiwa Mariam S. Faki, Mhesihmiwa Dr. Charles O. Mlingwa, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, ndiyo anayeongea, Mheshimiwa Filemon Ndesamburo, Mheshimiwa Mariam R. Kasembe, Mheshimiwa Hadija S. Ngozi, Mheshimiwa Juma S. Nh'unga, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mheshimiwa Ali Said Salum, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Aziza Ali, Mheshimiwa Lucy Owenya na Mheshimiwa Anastazia Wambura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, namshukuru sana Katibu wa Bunge, Dr. Thomas Kashilillah na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake. Aidha, shukrani za pekee zimetolewa kwa Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Yona Kirumbi, Grace Bidya na Michael Kadebe, kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuratibu shughuli zote za Kamati wakati wa kuandaa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Job Ndugai, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. RAJAB MOHAMMED SOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Mwalyosi kwa uwasilishaji wa hoja.

Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba nimwite Msemaji kwa upande wa Serikali ambaye ni Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia Mazingira, Mheshimiwa Dr. Batilda Buriani.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kuniwezesha kusimama hapa leo kujibu na kuchangia taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, kuhusu athari ya mazingira katika mgodi wa dhahabu wa *Barrick North Mara*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru wewe kwa kunipa fursa hii lakini pia nimshukuru sana Mheshimiwa Spika kwa busara zake na hekima kubwa katika kulishughulikia jambo hili na hasa pale alipoamua kwamba itakuwa bora na itakuwa vema kuwa na Kamati ambayo itashughulikia suala hili na kulipa jukumu Kamati Ndogo ambayo ilihusisha Wajumbe kutoka Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira pamoja na wale waliokuwa wanashughulikia masuala ya madini. Lakini hatma yake baada ya ziara hiyo, ni kumwachia Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Ardhi, Maliasili na Mazingira, kusimamia jukumu hili hadi hitimisho lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikiri kwamba Kamati ya Kudumu ya Bunge, Ardhi, Maliasili na Mazingira, imefanya kazi yake kwa uongozi na ushirikiano mkubwa na hatma yake ndiyo tumepata taarifa hii nzuri yenye kina na yenye mwelekeo ambapo kwa kweli kama Serikali, tunasema ni ripoti ambayo inatoa mwongozi katika utendaji na usimamizi wa masuala mazima ya mazingira hasa katika eneo zima la mazingira kama sekta mtambuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kusema kwamba Serikali inakubaliana na taarifa ya Kamati ya Bunge, Ardhi, Maliasili na Mazingira na kwamba imepokea taarifa hii na itatumia kama mwongozo kukamilisha shughuli zilizobaki katika kuhakikisha kwamba athari za mazingira zinaondolewa kabisa. Aidha, kama alivyoeleza Mwasilishaji wa Kamati, Serikali ilisimamia suala hili kwa uzito wa kipekee. Napenda niseme kwamba, ushirikiano tuliokuwa tukiupata kwa pamoja katika kushughulikia suala hili, ilituwezesha sisi kama Serikali kuweza kufuatilia mambo yetu katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niweze tu kupitia kwa kifupi katika yale maeneo ambayo Kamati ilitoa maagizo. Kimsingi, Serikali haina ubishi wala haina tatizo na ripoti kama nilivyosema na Serikali baada ya pale iliandaa Mpango Kazi na kutokana na maelekezo ya Kamati, tuliweza kubainisha hatua mbalimbali zinazotakiwa kuchukuliwa na zilizokwisha kuchukuliwa katika kipindi cha muda mfupi yaani Oktoba mpaka Desemba mwaka jana. Lakini vile vile katika kipindi cha muda wa kati ambao ni kuanzia Januari mwaka huu ulioanza hadi Juni mwaka huu, ni mambo yatakayotekelezwa katika kipindi cha bajeti cha mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipindi hivi vimegawanywa kwa kuzingatia mambo yafuatayo:- Kwanza, ni hatua za haraka zilizohitajika kuchukuliwa ili kuhakikisha kwamba

uchafuzi ambao ungeendelea kusababisha madhara kwa mazingira, binadamu na mifugo hautaendelea. Lakini vile vile kuchukua hatua ambazo si za haraka sana lakini zingeweza kutekelezwa katika bajeti ya mwaka huu zimefanywa na la tatu ni kuhakikisha kwamba hatua ambazo zinaweza kungoja kwa mwaka ujao wa fedha ili ziombewe fedha zinaweza kupangiwa. Mimi sitarudia yale ambayo Kamati kimsingi imeshayaelekeza na imeshatambua kama Serikali imefanya nini na Kamati imesharidhika. Lakini niseme tu kwa ujumla katika hatua hizo Serikali kupitia maagizo ya Kamati iliweza kufanikisha yafuatayo:-

Kwanza, ni kutenga maeneo kwa ajili ya shughuli za uchimbaji mdogo katika Mkoa wa Mara. Utekelezaji wake ni kwamba Wizara yetu ya Nishati na Madini, wamekwishatambua maeneo ya uchimbaji mdogo katika Mkoa wa Mara na *codes* zake zimeshachukuliwa. Maeneo yatakayotambuliwa, ni maeneo ya Itandulu katika Kijiji cha Nyakuguru na eneo la Goronga, Dibasa. Waziri mwenye dhamana ya madini ameshashauriwa kuridhia mapendekezo ya kutoa eneo hilo na suala hili sasa hivi linaendelea na timu ya wataalam kutoka Wizara ya Ardhi, imeundwa kwa ajili sasa ya kupanga, kutathmini na kupima maeneo haya ambayo yamebainishwa na kutengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile katika maagizo kulikuwa na suala zima la kufuatilia utekelezaji sasa katika maeneo mazima ya kisekta mfano kupata vyanzo vipya vya maji. Kamati alivyoeleza ni kwamba Wizara ya Maji na Umwagiliaji, tayari imeshabainisha vyanzo vya maji katika maeneo tisa. Lakini vile vile kulikuwa na umuhimu mzima wa kuhakikisha kwamba mwekezaji anaandaa mpango wa kuweza kuhakikisha anafuatilia sasa masuala mazima ya usimamizi wa mazingira na sisi kama Baraza kuweza kuwa na mpango wa siku zote wa ufuatiliaji. Mimi nasema katika utekelezaji wa hili pamoja na agizo la kuangalia sasa uzoefu huu ukapelekwa katika maeneo mengine ya migodi, tayari Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Wizara ya Nishati na Madini, Baraza letu la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira pamoja na Ofisi yetu ya Mkemia Mkuu, wamegawanya maeneo na wameshakwenda kupita katika maeneo mbalimbali ya migodi yetu. Kwa hivyo, migodi yote imeshapitiwa kwa maana ya ukaguzi wa awali na imebaki migodi miwili ambayo tunategemea kufanya ukaguzi wake katika kipindi cha mwaka huu. Lengo kwa kweli ni kuangalia uzoefu tulioupata katika kusimamia suala hili, litakuwa ni msingi wa kusimamia na kuepusha madhara ambayo yanaweza kutokea katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna suala zima la kuangalia jinsi gani sasa mgodi unaweza kulipa fidia na kuondoa wananchi walio katika maeneo hatari kandokando ya mgodi. Wizara ya Nishati na Madini, imeshafanya mawasiliano na mgodi na mpaka sasa watu 14 wanaopashwa kuhamishwa wamekwishatambuliwa. Utambuzi wa watu zaidi wanaotakiwa kufidiwa na kuhamishwa na vyote viwili kuhamishwa na kufidia, unafanyika na hili zoezi linatakiwa kuhitimishwa hivi karibu hususan katika maeneo ya Nyabirama na Gokona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile katika maeneo mbalimbali ambayo Kamati imetuagiza, kulikuwa kuna suala zima la kutoa taarifa kwa uma kuhusu matatizo yaliyojitokeza na hatua ambazo zinatakiwa kuchukuliwa. Suala hili lilikuwa Watendaji, waliona ugumu kidogo wa kutoa hili suala nje kwa jamii kutokana na kwamba taarifa ambayo ilikuwa inashughulikuwa ilikuwa haijatoka wazi kwa umma. Sasa tunategemea baada ya taarifa hii kupita katika Bunge hili, tutaweza kutoa taarifa na watendaji wetu katika ngazi za Kata, Wilaya, wataweza kueleza

wananchi kilichotokea na wataweza kutumia fursa hiyo kurudisha mahusiano na imani ya wananchi na kuweza kujenga mahusiano ambayo yatakuwa imara zaidi na kurudisha uhusiano ule ambao ulikuwepo awali kati ya mgodi pamoja na wananchi wa eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna suala zima la kuwa na umakini katika utafiti. Kamati imeeleza kuwa ni muhimu kuwe na utafiti wa kina katika masuala ya kiuchumi na kijamii katika maeneo yanayozunguka mgodi. Wizara ya Nishati na Madini, tayari imeshaandaa hadidu za rejea ya Mtaalam Mwelekezaji na mchakato wa kumpata Mwelekezaji huyu, unaendelea na sisi tunachukua maelekezo ya Kamati kwamba katika kufanya hili tutahakikisha tunasimamia suala hili na masuala mazima ya wananchi kuweza kufaidi rasilimali katika maeneo yanayowazunguka na yatapewa kipaumbele. Sisi kama Serikali tunaona kwamba taarifa hii ya masuala ya uchumi na ya kijamii, itakuwa ni msingi mzima katika kuona jinsi gani kwa siku za usoni wananchi wataweza kunufaika na rasilimali katika maeneo hayo. Kwa hiyo, suala hili tunazingatia na mchakato upo na litakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia mapitio ya Sheria ya Madini kuhusu fidia na shughuli za uhamasishwaji yaani uhaulishaji *compensation* na *resettlement.* Wizara ya Nishati na Madini, ilifanya zoezi la kukusanya maoni kutoka kwa watu, kwa madhumuni ya kuandaa Sheria mpya na wamefanya mikutano mbalimbali, shughuli hii ilifanyika Arusha kama ilivyopangwa tarehe 16 mpaka 18 Desemba mwaka jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile kuhusu fidia, wadau wameshauri viwango vya fidia vipangwe kulingana na aina ya uwekezaji rasilimali iliyopo katika eneo hilo. Kama mtakavyojua Sheria ya Fidia ambayo tunaifuata ni Sheria ya Fidia inayotokana na Wizara ya Ardhi na Sheria hii, kwa kweli ina fidia kulingana na mazao yaliyopo katika eneo lile. Sasa tumepata maoni ya wadau kwamba tuangalie sasa uwasilia na umuhimu wa kuangalia rasilimali iliyopo katika kutoa fidia. Sasa Wizara ya Nishati na Madini imechukua wazo hilo.

Aidha, wadau pia walipendekeza kwamba wananchi watakaohamishwa kupisha shughuli za migodi licha ya fidia wajengewe makazi mapya ambayo ni bora. Hili pia limechukuliwa na Serikali na kuona ni kwa jinsi gani tutaliingiza katika mchakato mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua iliyofuata ilikuwa ni kupata maoni ya Kamati ya Kudumu ya Fedha, ambayo sasa hivi tumeyapokea na kupitia kikao kilichofanyika Bagamoyo tarehe 18 na 19 mwezi wa jana. Tumeweza kupata maoni ambayo pia kimsingi sasa hatua inayofuata ni kuandaa Muswada wa Sheria ambao unatarajiwa kuwasilishwa katika Bunge letu mwezi wa nne mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kufanya ukaguzi wa migodi, kama nilivyokwishaeleza, ili kubaini athari zake katika mazingira na hili nimesema kwamba migodi yote ukitoa migodi miwili ya Rezoleti na Kabanga, ndiyo imepangiwa kwa kipindi cha mwaka huu. Lakini migodi mingine kama Rezoleti, Mwadui na maeneo mengine ya Buzwagi, North Mara, Kiwira, Bulyanhulu, GGM na *Geita Gold Mine*, yote hiyo imekwishafanyiwa ukaguzi na tunaona kwamba ukaguzi huu sasa utakuwa ni ukaguzi ambao unaendelea. Timu ya pamoja ambayo Serikali iliunda kuhusisha sekta na taasisi mbalimbali, itaendelea kuwa ndiyo timu ambayo itakuwa inafanya kazi kwa pamoja na sisi tumeona zoezi hili limetuimaimarisha zaidi

katika uratibu na inatufanya sote tuwe pamoja kwa sababu mambo haya yanapotokea yanakuwa ni matatizo ambayo yanazigusa sekta mbalimbali. Kwa hiyo, zoezi hili litakuwa ni zoezi ambalo litakuwa ni la kudumu kuzunguka katika migodi, kutumia wataalam kutoka hizo sekta ambazo ziliguswa na kadhia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilielekeza umuhimu wa kujenga majosho na kushughulikia masuala ambayo yalionekana kuwa ni kero na kubainisha vyanzo salama. Kama nilivyosema, kwa maana ya vyanzo vya maji, tayari Wizara ilibainisha maeneo tisa na kushirikiana na Mhandisi wa Maji wa Wilaya ya Tarime. Usanifu na ukadirishaji wa gharama za ujenzi wa mradi, unaendelea. Vile vile Wizara imefanya upembuzi yakinifu kubaini maeneo ya ujenzi wa majosho na malambo ambayo gharama halisi inayohitajika imewekwa katika mchakato mzima wa hii *table* au jedwali ambalo tumeliambatanisha katika ripoti yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo ambayo yamepangiwa utekelezaji wake katika kipindi hiki cha fedha kinachokuja, Wizara ya Maji, imeangalia maeneo ambayo yataweza kukarabatiwa na kuongezewa fedha zaidi ambayo ni maeneo ya Nyakuguru, Nyaruana, Nyangoto, Matongo, maeneo ya Kewanja, Weijita hii ni pamoja na kuweka masuala mazima ya majosho. Lakini vile vile kulikuwa na vijiji vya Nyakaguru, Gibaso, Weigita, tukaona kwamba ni vizuri pia vikatumia fedha zile ambazo ni za *DADPs* kwa mwaka huu jumla ya shilingi 8,000 zilihitajika na ambazo zingeweza kufanya hiyo kazi na jumla ya shilingi za Kitanzania milioni 235 zimepangwa kwa ajili ya Nyakaguru lakini vile vile jumla ya shilingi milioni 28 zinahitajika kwa ajili ya Jibaso na Weigita, shilingi milioni 22.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magonjwa tunasema kwamba utafiti wa magonjwa ya mifugo umeendelea na utaendelea katika kipindi hiki kinachokuja kuweza kuona kwamba utafiti wa kina unafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na agizo la kudhibiti uingizwaji holela na matumizi yasiyo sahihi ya masuala mazima ya zebaki katika uchimbaji mdogomdogo na hii tunasema kwamba Mkemia Mkuu aliweza kusimamia suala hili pamoja na *TRA* na hivi linashughulikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna masuala mengine ambayo yalielekeza kuhusu kufanya uchunguzi wa wingi na ubora wa vyanzo vya maji. Hili tumelielezea na tumesema kwamba kuna visima 18 vitakavyochimbwa katika vijiji saba na ambavyo vimekadiriwa kugharimu shilingi milioni 255 na kazi ya mradi huu itaanza mwezi wa tatu mwaka huu, baada ya Makandarasi kupatikana na kushirikisha Halmashauri ya Wilaya ya Tarime. Wilaya kwa kushirikiana na Serikali za Kata na Vijiji, itaweka mfumo endelevu wa ufuatiliaji wa afya ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya, imetenga shilingi milioni 8.4 kwa ajili ya uzoaji wa taka kwa mwaka huu, katika miji midogo ya Nyamongo, Kivunge na hii ni kwa kutumia ile *incinerator*. Lakini vile vile *incinerator* itanunuliwa moja na Afisa Afya wa Tarafa anatakiwa kusimamia kikamilifu shughuli hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunasema pamoja na matatizo haya, zoezi hili limetuwezesha kuibua matatizo mbalimbali ambayo yalikuwa yanaikabili Wilaya hiyo, kwa mfano matatizo ya kiafya, kulikuwa kuna uhaba wa wataalamu na Wizara imeagiza kwamba Wataalamu hao waweze kupatikana na kuweza kuajiriwa kulingana na bajeti yao. Sasa niseme tu kwamba hayo ni mambo ambayo tayari yameshafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna maagizo ya msingi, kwa mfano kulikuwa kuna Agizo Namba 2, kwamba Wizara ya Nishati na Madini imepokea agizo hilo na hivi sasa suala zima la kuweza kuwawezesha wawekezaji waendelee na utekelezaji wa mapendekezo hayo inakamilishwa. Hii *Task Force* kama nilivyoeleza ya kuhakikisha kwamba Mkaguzi anafuatiliwa kuhakikisha kwamba taarifa za utafiti na ukaguzi zinakuwa ni taarifa zetu wenyewe, tunasema kwamba utafiti tulioufanya na kwa kuanzia na ukaguzi tuliouanza tumejenga *data base* ambayo kila mwaka tutakuwa tukifanya ukaguzi kwa kutumia taarifa ambazo tulikuwanazo. Kiutaratibu, kama tunavyofanya tathmini ya athari kwa mazingira, huwa mwekezaji ndio anafanya tathmini, Baraza linafanya upembuzi na kuthibitisha. Katika maeneo haya nyeti, tunaona ni vizuri na sisi tukaweza kujiridhisha kwa kuweza kufanya tathmini yetu ya kina ili kuweza kulinganisha tunayoyapata na yale ambayo watayaleta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna suala zima la Agizo namba 3, ambapo Kamati imeagiza kwamba kuwe na maeneo ya wachimbaji. Kama nilivyosema ni kwamba maeneo hayo yameshapangwa na yatazingatiwa. Kufutatia migogoro mbalimbali iliyokwishajitokeza na masuala mazima ya fidia, tumeshaeleza kuwa ni muhimu kuona kwamba sasa hivi eneo linapimwa lakini Wizara kufuatilia ili kuona kwamba wale ambao bado hawajahama katika eneo ambalo lilitakiwa lizungushiwe uzio ili watoke katika eneo lile la mgodi, hasa ukizingatia kwamba jiografia na ikolojia ya mgodi wa *North Mara*, ni tofauti na migodi mingine, linaendelea. Sasa hivi tunaona kwamba sheria hii itakapopitishwa itawezesha na itaipa nguvu zaidi Wizara kuweza kufikia hatma ya mgogoro huu. Mara baada ya kubainisha kiwango cha fidia, basi wale ambao hawatataka tena kutumia kile kiwango basi sheria itatumia hatma yake ili kuepusha athari ambazo zinaweza kutokea kwa wale watu kukaa karibu na meneo yale ya mgodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla sisi tunasema kwamba mapendekezo ya Kamati kuimarisha taasisi na sekta mbalimbali za Serikali ni ya msingi sana, kwa sababu sasa hivi suala la mazingira ni suala ambalo limeanza na limekuwa likipata ufahamu na kupokelewa na wananchi kwa kiwango kikubwa sana. Tunasema kwamba wananchi wameweza kuwa chachu ya kutuletea changamoto kubwa ya baadhi ya athari ya mazingira inayoendelea katika maeneo yao. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru sana wananchi pale wanapoona matataizo mbalimbali ya kimazingira kuweza kuripoti Serikalini na kupitia vyombo vya habari ili sisi tujue na hatua zitachukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile niseme kwamba changamoto hii inakuja na changamoto nyingine ya kuweza kulijengea uwezo kama Kamati ilivyosema. Sisi tunajua kwamba Baraza letu na ukiangalia ukubwa wa nchi yetu, bado tuna wataalamu ambao ni wachache sana; Wataalamu Wakaguzi wa Masuala ya Mazingira kwa nchi ndogo kama Sychelles wanafika 40, Wataalamu Wakaguzi wa Mazingira Kenya sasa hivi lengo lao ni kufika 1,000. Sisi Tanzania sasa hivi tuna Wakaguzi 20 tu wa mazingira, kwa hiyo, bado tuna

Wakaguzi wachache sana na rasilimali ndogo sana kuwezesha taasisi yetu kufanya kazi hii. Tatizo hili lilipotokea, haikuwa ndani ya bajeti ya Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, lakini kwa sababu ilikuwa ni dharura, Baraza ilibidi kuweza kulichukulia suala hili na kuweza kufanya kazi kama ilivyotakiwa. Hili pia limetupa uzoefu kwamba katika bajeti inayokuja, tuweke fedha za kutosha katika masuala haya ya tafiti na ufuatiliaji, kwa sababu, ni jambo ambalo sasa litakuwa likifanyika mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana Kamati kuliona hili; hatuwezi kubisha wala hatuwezi kusema kwamba Baraza lina nguvu na uwezo wa kukidhi matatizo ya nchi hii na ukubwa wake, Baraza mpaka sasa hivi lina ofisi katika Kanda zetu nne tu; Kaskazini, Kanda ya Kusini, Kanda ya Ziwa na Kanda ya Pwani ambayo ni pamoja na *Head Quarters* pale. Sasa ukichukulia matatizo yanayopatikana katika nchi nzima, Baraza halina uwezo. Tunaomba tutumie fursa hii na ninyi mtusaidie katika kipindi hiki tuweze kulipa nguvu Baraza liweze kusimamia masuala mazima ya ufuatiliaji na uboreshaji wa mazingira katika miji yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na Kamati kwamba mchakato wa kufanya tathmini ya athari ya mazingira katika maeneo ambayo migodi na wachimbaji wadogo wadogo watakayopewa, liwe ni jukumu la Serikali. Sasa hili tutashirikiana na wenzetu wa Wizara ya Nishati na Madini, kuona kwamba suala hili tunalifanya vizuri ili liweze kufanyika kwa wepesi zaidi. Lengo pia la kupitia Sheria yetu ya Mazingira, ili kuanzisha Mfuko wa Mazingira; tunategemea kuzindua Mfuko huu ndani ya kipindi hiki cha *quarter* hii ya kwanza ambapo Mfuko wa Mazingira wa Taifa utazinduliwa pamoja na kazi nyingine za fedha za mfuko huo, sio tu kutoa elimu lakini ni kufanya shughuli hizi za ufuatiliaji wa masuala mazima ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikiri kwamba zoezi hili limetuhamasisha na limetupa uzoefu ambao tutauimarisha na tutausimamia katika usimamizi wa mazingira katika maeneo ya migodi kama nilivyosema. Aidha, Serikali kupitia ile timu ya wataalamu ya kisekta, itaendelea kufanya kazi kwa pamoja katika kukagua migodi katika maeneo yaliyobaki lakini pia kurudi katika maeneo yale ya awali na kuweza kukamilisha ripoti hiyo. Ripoti ya Serikali ya hatua mbalimbali za ufuatiliaji, ikiendana na tarehe ya kukamilisha hatua hizo, itawasilishwa kwa Kamati kama ilivyoelekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda nichukue fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Mawaziri wenzangu wa kisekta, ambao tumeshirikiana nao katika kushughulikia tatizo hili. Napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Profesa David Homeli Mwakyusa, Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na Naibu wake wa Afya, Dokta Aisha Kigoda. Napenda nimshukuru Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Waziri wa Maji na Umwagiliaji pamoja na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Injinia Chiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nimshukuru sana Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, Waziri wa Nishati na Madini, pamoja na msaidizi wake Mheshimiwa Adam Malima. Napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Dokta John Magufuli, Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Dokta Wanyancha. Halikadhalika, napenda kuwashukuru sana Mheshimiwa Kanali Mstaafu Mafuru, Mkuu wa Mkoa wa Mara na

Mheshimiwa Frank Luhahula, Mkuu wa Wilaya ya Tarime, kwa ushirikiano mkubwa waliotupa katika zoezi zima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue fursa hii pia niwashukuru wataalamu wote wakiongozwa na Katibu Mkuu, Bibi Ruth Molel, Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Hifadhi ya Usimamizi wa Mazingira pamoja na sekta zote ambazo zilihusika katika mchakato huu mzima, kwa ushirikiano mkubwa na taarifa muhimu zilizowezesha Kamati hii ya Bunge kuweza kufanya kazi yake vizuri. Pia kipekee, napenda nirudie kuipongeza Kamati hii kwa ujumla, ikiongozwa na Mheshimiwa Job Ndugai, kwa ushirikiano mkubwa na kwa ripoti hii nzuri ambayo kwa kweli Serikali imeipokea kwa moyo mkunjufu sana. Vilevile niwapongeze wajumbe wote, lakini kipekee nimpongeze Mbunge wa Jimbo la Tarime, kwa ushirikiano wake mkubwa katika zoezi hili lote hadi tukafikia hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kusema kwamba Serikali inaunga mkono na inaipokea ripoti hii. Tutaendelea, kama ulivyoagiza, kutoa taarifa za utekelezaji wa mara kwa mara pamoja na jedwali ambalo tumeliandaa likionesha utekelezaji wa maeneo ya kati na maeneo yale ya muda mrefu ambayo yatakuwa yakiendelea. Naomba kushukuru na kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu Utaratibu.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68. Kwa mujibu wa Kanuni ya 114 (17), baada ya Taarifa za Kamati kutolewa kutakuwa na mjadala lakini utaratibu uliotumika leo baada ya Mheshimiwa Waziri kutoa maelezo hayo, sisi tutasema nini tena? Naomba muongozo wako.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, hii hoja sio ya Waziri, hii hoja ni ya Kamati. Kamati imetoa hoja yake, Waziri aliyezungumza sasa hivi ni wa sekta ambayo inahusiana na hii hoja iliyotajwa. Kwa hiyo, alikuwa na haki ya kimsingi kuwa mtu wa pili hapa kuzungumza. Baada ya yeye, Waheshimiwa Wabunge watafuatia kuchangia, huzuiwi kuchangia. Najua inawezekana kaku-*pre-empty*, Waziri kataja kitu ambacho ulikuwa unataka kukizungumzia lakini kama unafahamu zaidi unaweza ukazungumza kwa sababu nafasi utaipata ya kuongea kwa wale ambao wameomba. *(Makofi)*

*Actually* nimesimama niwaambieni kwamba mpaka sasa hivi, nina watu saba walioomba kuchangia na nitawaruhusu wachangie. Wapo Mawaziri watatu watakuja kuzungumza baadaye baada ya wajumbe saba kuchangia. Kwa hiyo, tutaendelea na utaratibu kama kawaida, nitawaita kwa utaratibu ufuatao. Ataanza Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Luhahula na baadaye Mheshimiwa Charles Mwera ajiandae na wengine watafuata. Baada ya hapo mwisho kabisa nitakuwa na Mawaziri watatu, kutakuwa na Waziri wa Nishati na Madini ambaye naye ataongea kwa sababu na yeye imemgusa, kuna Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji ambaye ataongea hapa vilevile pamoja na Waziri wa Afya; hao wote

watazungumza mwisho baada ya wajumbe kuchangia. Baada ya hapo, nitamruhusu Mwenyekiti ambaye amekuja kutoa ile hoja kuja ku-*respond* kwa yale ambayo yametolewa na Serikali na yale ambayo mtayachangia ninyi Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Pamoja na hivyo Waheshimiwa Wabunge, kuna nyongeza ya shughuli za Bunge kwa siku ya leo. Nadhani *Order Paper* mpya imeshatolewa, mtaona kwamba kuna nyongeza ya shughuli kwa siku ya leo, kwa maana ya kwamba Bunge litaendelea mpaka jioni.

Baada ya maelezo hayo machache na ninashukuru kwa hiyo hoja uliyoitoa Mheshimiwa Mbunge, naomba sasa nimwite Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri ili aanze kuchangia.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii, kukushukuru kwa kunipa nafasi niwe mchangiaji wa kwanza katika hoja hii ambayo inahusu Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu athari za mazingira za mgodi wa dhahabu wa *Barrick, North Mara.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi tajiri sana, ina wingi wa rasilimali, rasilimali hizo ziko kwenye ardhi, ziko kwenye maziwa na bahari na kwa kweli Tanzania kama nchi, inayo haki ya kuzitumia rasilimali hizi ili iweze kufaidika nazo. Zipo nyingine imewaachia wananchi wa Tanzania ili wenyewe waweze kuziendeleza, lakini zipo nyingine ambazo kwa ajili ya uzito au ukubwa wa mtaji unaotakiwa basi inatoa nafasi kwa wawekezaji wengine mbalimbali walio ndani ya nchi ama wa kutoka nje ya nchi kuweza kuendeleza rasilimali zetu kwa lengo la kupata manufaa makubwa kwa ajili ya nchi kama nchi lakini pia kwa ajili ya wananchi wote, Mtanzania mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ndipo linapoanzia tatizo ambalo linatupeleka kwenda kujadili athari za mazingira katika mgodi wa *North Mara.* Mgodi huu ni maliasili mojawapo ya Tanzania ambayo Mwenyezi Mungu ametupatia, lakini tunaona kwamba katika ile hali ya kuweza kupata mali hii kwa ajili ya faida ya Watanzania, kuna mambo mengi ya msingi ambayo hayakuzingatiwa. Ninapenda kusema kwamba hili sio tatizo la kwanza linalohusu matatizo ya migodi au matatizo ya uwekezaji katika nchi yetu hii kufika ndani ya Bunge hili Tukufu na kujadiliwa wazi ndani ya kikao hiki, isipokuwa nadhani kumekuwa pengine na kutokufuatilia mara kwa mara baada ya mijadala, kwa hiyo, yameendelea kujirudia kama vile ni suala jipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niseme kwa namna moja au nyingine, ninapata faraja kwa sababu ninaona kuna namna ambayo katika maagizo ya Kamati imetoa agizo moja ambalo limenipa faraja kwamba kuwe na ratiba ya utekelezaji wa kupunguza athari hizi au kuziondoa kabisa ambayo mwekezaji amepewa lakini bila ya shaka ni lazima na Serikali yenyewe ifuatilie kwa karibu ili maagizo hayo yaweze kuwa ni ya manufaa kwa Watanzania. Sisi wote tunapenda kuona kwamba Taifa letu linasonga mbele na unafika wakati wa kuwa hata na bajeti inayojitegemea. Lakini katika harakati hizi, ningefarijika sana kama ningesikia pia kuwa hata Watanzania wenyewe mmoja mmoja na hata kwa makundi wanafaidika na harakati hizi kwa sababu kama tunakuwa na mkataba ama tunakuwa na mwekezaji ambaye uwekezaji wowote ule ambao tunakuwa nao hauwezi kumfaidisha mwananchi mmoja mmoja ambaye ni mwenyeji katika eneo linalohusika, ni lazima mgogoro utajitokeza. Migogoro hii ya mara kwa mara kwa namna moja au nyingine hata haki za binadamu zinakuwa hazizingatiwi lakini wakati mwingine

inaonekana kwamba pengine wananchi katika eneo lile na wenyewe wanaonekana kama ni sehemu ya mali sio sehemu ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi ninasema kwa sababu hili halijajitokeza kwa mara ya kwanza, tunaendelea kuliona na ni vema kabisa tunapokuwa tunakwenda kuweka mkataba na wawekezaji wowote, wawe wanawekeza kwenye migodi, wawe wanawekeza kwenye samaki, wawe wanawekeza kwenye uendelezaji wa mifugo, wawe wanawekeza katika kitu chochote ambacho kinakuja kufanyika katika kundi ambalo wao hawakuwa wenyeji pale ila wamepewa waende wakachukue rasilimali ya pale na kwa sababu wana mtaji mkubwa, ni lazima ndani ya mkataba wao kuwe na vitu vya msingi ambavyo ni lazima vifanyike, wavifanye wao kwa kuwanufaisha wananchi wa lile eneo, wananchi wenyeji wakazi wa lile eneo. Kwa mfano vitu kama maji, inasikitisha wawekezaji wanapopata kibali wanakimbia kwenda kuweka uzio katika lile eneo bila kujali kwamba vitu kama maji viko kwenye eneo ambalo wao wanakwenda kuchukua mali ile, wenyeji walikuwa wanategemea maji hayo hayo. Kwa hiyo, wanazingira maji na kuwekea ulinzi mkali bila kujali waliokuwa wanakaa pale walikuwa wanayategemea maji haya haya. Sasa hili ni tatizo ambalo ni lazima tuhakikishe kwamba hii haiwezekani, kama watu wanakwenda kutumia maji waliyoyakuta pale imekuwa ni sehemu ya eneo walilopewa ni lazima sasa wahakikishe kwamba kule nje wanachimba kisima kingine ambacho kitaendelea kuwasadia wale watu ambao wanatolewa kwenye lile eneo ili waendelee kupata huduma ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna vitu vingine ambavyo pia ni muhimu, unakuta mwekezaji anakwenda kuwekeza ndani kabisa *interior,* lakini hata barabara itaendelea kuwa ni ile ile ya miguu ya ng'ombe ambayo haifai. Lakini yeye anakwenda kuchukua mali yetu na kuondoka lakini wananchi wanaendelea kubaki hawana hata barabara. Kuna vitu vingine muhimu kama shule, mwekezaji anapofika pale yeye kwa muundo wa Taifa letu maeneo mengi yako chini ya vijiji, sasa yeye akishapewa kile kibali cha kwamba anamiliki lile eneo ambalo ama lilikuwa chini ya kijiji ambacho sasa wanakijiji wanatolewa nje basi yeye anajiona mgeni, Mungu mtu mdogo; badala ashirikiane na wananchi katika maendeleo na kujiona kwamba ni sehemu ya kijiji anaanzisha mgogoro. Sasa hii migogoro utakuta kwamba ndio inayopelekea malalamiko mengi ya wananchi, hawezi kuwasaidia katika ulinzi na usalama badala yake analeta Maaskari wake wenye silaha na bunduki na vitisho, hata njia walizokuwa wanapita wananchi kwenda katika maeneo yao zinazibwa, mtu akijaribu kupita, silaha, akijaribu kueleza anaambiwa hili eneo liko chini ya ulinzi na liko chini ya mwekezaji, hii haiwezi ikatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakusudia kuona kwamba uwekezaji huu ni kwa manufaa kwetu, ni kwa manufaa ya Taifa na wananchi mmoja mmoja. Huyu mwekezaji ahakikishe kwamba ameshirikiana na wananchi kuhakikisha wamepata shule, kwa mfano, kama amekuta shule yao ni mbaya, shule yao iwe nzuri, kama amekuta hawana zahanati, wawe na zahanati kusudi afya zao ziboreke. Kama amekuta pale wana shida nyingine ambazo kimsingi ni huduma zao ambazo walikuwa hawajazipata wakiwa peke yao, leo hii nguvu iliyoingia ya mwekezaji mgeni lazima ioneshe tofauti kwa wananchi kwanza vinginevyo tunapoendelea kufikiria kwamba amelipa Taifani, migogoro hii haitakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kwamba ni lazima uwekezaji wetu wa namna yoyote ile ulenge kuhakikisha kwamba unanufaisha wananchi na hakika ni lazima Serikali ifuatilie, iwe na kipindi cha kufuatilia mara kwa mara, ikihakikishe kwamba uwekezaji unaleta

amani, unaleta faida kwa nchi, lakini amani na utulivu na upendo kwa watu ambao wako pale ni vya lazima. Mimi ninafurahi kuona kwamba uwekezaji unaonekana kwamba unaunganisha mwenyeji mkazi na mgeni na wao wanaona kwamba sasa sisi wote ni binaadamu, hata kama ni wa Mataifa tofauti lakini sisi wote ni binadamu. Badala ya kukaa katika hali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapoyasema haya ninayazungumza kwa uzoefu. Kwenye Jimbo langu nina wawekezaji wa mifugo, lakini badala ya kuja wakiwa ni marafiki wamekuja na vitisho. Hali hii imesababisha mgogoro na hata sasa mgogoro upo tu kwa kauli ya Serikali kwamba hebu tulieni tunatatua mgogoro, lakini hawahusiki. Wamewanyang'anya wananchi maji, wamewawekea ulinzi unaotisha, vipigo kila wakati, hakuna barabara, hakuna zahanati, ni hali ambayo inatisha na hali ya namna hii mimi ninaona kila wakati tutaendelea kuleta malalamiko. Ninaomba mambo haya yazingatiwe, kwa kweli matatizo haya yasiendelee kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama inalazimika basi wananchi wanaondoshwa katika eneo lao, fidia ya kutosha iwepo. Fidia hii mimi ninaomba isiangalie tu mazingira kwamba huyu alipo hapa kulikuwa na maliasili kwa hiyo yeye apewe pesa kubwa, huyu alipokuwa kulikuwa na shamba tu amepanda miti miwili aah, aah, fidia iwe ni fidia kama mtu wamemwondoa kwenye eneo lake fidia ilingane, kwa sababu huwezi kunitoa kwenye nyumba ya majani ukanilipa nikajenge tena nyumba ya majani. Unaponiondoa kwenye nyumba ya majani maana yake unaniwezesha kwenda kujenga nyumba ambayo sasa itakuwa ni nyumba yenye bati, nyumba nzuri, kwa sababu nimepata mwekezaji. Kwa hiyo, fidia zilenge kwamba zinakwenda kuboresha hali ya wananchi. Walipoondoka pa kwanza na wanapokwenda kwa mara ya pili, pawe ni pakuwawezesha kuhakikisha kwamba sasa wanaboresha maisha yao. Mimi ninadhani haya ni masuala yanayolenga kubadili hali za Watanzania; hayalengi tu kwamba tuna shida ya pesa, tunashida pia ya kuona hali za Watanzania kimawazo na kiutekelezaji ilenge kwamba kuna kitu kipya ambacho kimefika kwetu na kitu hiki ni kwa manufaa yetu sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali kwamba kwa wale wachimbaji wadogo wa kule *North Mara*, ambao wametakiwa kupewa maeneo ya kuchimba, hili wala lisiwe ni la kuchelewa, lifanyike haraka. Lakini mrahaba unaotakiwa kulipwa kwa Halmashauri, utosheleze na ulenge kusema kwamba tunalipa mrahaba huu ufanye nini; sio kwamba wanapewa *token money* kusudi ionekane kwamba kuna kipesa kidogo wamepewa, hapana, wanatoa pesa hizo zifanye nini? Mwaka huu wanajenga shule, ijengwe. Mwaka ule wanatengeneza barabara gani, ijulikane. Mwaka huu wamejenga zahanati kijiji fulani, ijulikane. Kuwe na kitu ambacho huo mrahaba wa kila mwaka uwe una kitu ambacho kinakusudiwa kufanyika ili baada ya muda, unaweza ukasema mwaka huu walitufanyia hiki, mwaka huu walifanya hiki, walifanya kile. Haya madini yetu sisi yanakwisha, yatakapokuwa yamekwisha hatuwezi kubaki hatuna kitu chochote halafu tunasema tulikuwa na watu wanalipa mrahaba, hata! Ni lazima hata watoto wetu ambao tunapochimba madini haya hawajazaliwa, watakapokuwa wamekua waseme pale tulijengewa na watu wa madini, pale tulijengewa na watu wa mifugo, pale tulijengewa na watu wa gesi, yaani kila kitu ni lazima kionekane kwamba tunaweza tukasema hapa tulipata wakati tulipokuwa na kitu hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nipende kusema kwamba ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii na ninaunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa sababu ametuwezesha kuwepo siku ya leo. Lakini niipongeze Kamati kwa taarifa yake waliyotoa hapa Bungeni kwa siku ya leo, lakini nipongeze majibu ambayo Mheshimiwa Waziri, alikuwa anajibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la uwekezaji, ni tatizo la *North Mara,* tusipoliangalia katika maeneo mbalimbali katika Taifa letu, linaweza likaleta usumbufu mkubwa sana katika baadhi ya maeneo. Ukiangalia katika maagizo mbalimbali ambayo yametolewa na Kamati, yako maeneo ambayo ninaomba niishauri Serikali. Kuna agizo la kutafuta ufumbuzi au upatikanaji wa vyanzo vya maji haraka, wamesema kwamba Serikali imefanya tathmini na imekadiria shilingi milioni 250 zinazoweza kutumika kuleta maji kwa haraka katika eneo hilo. Pia wamesema kwamba wanaangalia uwezekano wa kushirikisha mwekezaji. Napenda kushauri Serikali, nafikiri katika hili si vizuri sana kuchelewesha upatikanaji wa maji kwa sababu tayari maji yaliyoko pale, yameshaathirika na wananchi hawa wapo na shilingi milioni 250 sioni tatizo sana kwa Serikali kuhakikisha kwamba wananchi wanapata visima haraka sana katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna suala la fidia kwa wananchi wanaozunguka maeneo ya uwekezaji. Safari moja katika Bunge hili Tukufu, nilisema ili tuweze kuwafaidisha wananchi wetu katika kuwafidia maeneo yao, ni vizuri sana zoezi la kurasimisha ardhi lifanyike kwa haraka sana. Kwa sababu hata tunapoenda kutathmini maeneo, wananchi wale hawajarasimishwa ardhi yao katika maeneo yale, bado fidia yao inakuwa ndogo lakini tukirasimisha ardhi wananchi tutawapa uwezo na uhalali wa kupata fidia kubwa katika maeneo yale. Kwa hiyo, ni vizuri sana turasimishe ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafikiri Serikali ni vizuri katika bajeti yake inapotenga, au kwa mfano sasa hivi tumesema hata kuna suala la kilimo kwanza, hatuwezi tukalifikia kwa haraka wakati wananchi hawajarasimishwa ardhi zao, tukisharasimisha ardhi watakuwa na vibali na haki ya eneo lao. Lakini leo unamkuta pale, unamtoa kwa sababu hilo eneo kwanza hajalimiliki, unamwambia mwananchi yule ondoka, unampa fidia kidogo, kifuta machozi lakini kama ardhi ile amesharasimishwa anakuwa na haki nayo. Kwa hiyo, naishauri Serikali itenge fedha ya kutosha kurasimisha ardhi katika maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mahusiano bado halijawa zuri sana, tarehe tatu mwezi huu, niliuliza swali hapa na nikauliza mahusiano ya wawekezaji wakubwa pamoja na wananchi hasa wawekezaji wa migodi, mahusiano yao na wananchi katika maeneo yanayowazunguka sio mazuri sana. Mimi ninaweza nikatolea mfano katika mgodi wa Tulawaka ambao uko Biharamulo lakini huduma zao za jamii wanazipata katika Wilaya ya Bukombe, eneo la Runzewe, anatibiwa pale, barabara kama alivyosema mchangiaji aliyepita, wanatumia barabara ile ya kutoka mgodini Tulawaka kuja Runzewe.

Ukifika leo barabara ile ni mbovu sana, wawekezaji wale huoni wanachochangia katika Halmashauri ya Wilaya Bukombe au katika Kata husika. Ulipuwaji wa miamba ulikuwa unafanyika katika Kijiji cha Busozo, lakini hakuna chochote wanachokipata. Kwa hiyo, nafikiri Serikali hapa ni vizuri iliangalie suala hili. Tarehe 29 Desemba, 2009 nikiwa katika Kijiji cha Ruzewe pale Uyovu, walikuja FFU na walianza kulipua mabomu ya machozi, baadhi ya

wananchi wakanifuata wakaniambia Mheshimiwa Mbunge kuna FFU pale wanalipua mabomu wanawapiga wananchi; nilipofuatilia nikaambiwa kwamba, walikuwa wanawasaka wachimbaji wadogo wadogo eti huwa wanaiba mawe Tulawaka. Nilipojaribu kuongea nao, nilipowafuata nikawauliza mbona mnatumia nguvu kubwa kiasi hiki; ina maana mahusiano ya wananchi na migodi ile bado ni mibovu.

Kwa hiyo, hata siku ile nilipofanikiwa kuongea nao, mimi nilikwenda na gari langu likiwa linapeperusha bendera ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, askari wale wa FFU wanasema toa gari lako tutalilipua. Mimi nikasimama nikawaambia mwenye uwezo afanye, lakini nikasema ninataka nikutane na mkuu wa msafara. Namshukuru sana RCO wa Mkoa wa Kagera, ndiye aliyejitokeza tukaongea naye na nikauliza kwa nini mnatumia nguvu kubwa kiasi hiki mpaka tunawatisha wananchi hapa wanasema wananchi wa hapa wanaiba mawe Tulawaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukiangalia kwa namna ile, uhusiano wa wananchi na wawekezaji hauwi mzuri kwa sababu hata sasa hivi, leo Kamati ikisema iondoke itembelee eneo la Ruzewe ikakutane na wananchi, hawawezi wakakubaliana mahusiano ni mabaya. Kwa hiyo, tunaomba tuboreshe tatizo linalosababisha hili ni nini; linalosababisha hili ni utengaji wa maeneo ya wachimbaji wadogo wadogo. Naipongeza Serikali kupitia Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, jitihada alizozichukua wameshaanza kutenga maeneo, kwa mfano, Nyarugusu na maeneo mengine. Tunapotaka kuweka uwekezaji katika eneo fulani ni vizuri hapo hapo tunapoweka mwekezaji na wachimbaji wadogo wawe wamewekewa eneo lao. *(Makofi)*

Kwa mfano, ukiangalia labda eneo la Buzwagi, sidhani kama wachimbaji wadogo wadogo wametengewa eneo hata Bulyanhuru, lakini hata Bukombe, Wananchi wa Bukobe ni wachimbaji wadogo wadogo lakini bado maeneo hawajatengewa. Sidhani kama Wananchi wa Bukobe wanaweza wakaondoka waende Rwamgasa au Nyarugusu, kwa hiyo, naishauri Serikali iongeze kasi ya kutenga maeneo ya wachimbaji wadogo wadogo. Hawa wawekezaji washirikiane na wananchi katika huduma za jamii, kwa sababu tusipofanya hivyo, bado tunaweza tukajikuta kwenye matatizo sana. Ndio maana nawapa pole Wananchi wa North Mara, kwa uvumilivu ambao wamekuwa nao, lakini kwa nini Serikali tunasubiri mpaka tupate dharura ndipo tuanze kuchukua hatua. North Mara imetokea shida hiyo, tayari sasa tumeshaanza kutafuta vyanzo vya maji, tumeshaanza kuweka maeneo yao, kwa nini tusichukue tahadhari mapema, tutafute maeneo Buzwagi, tutafute maeneo Bulyanhuru, tutafute maeneo Bukombe, tutafute maeneo sehemu mbalimbali kabla dharura hizo hazijatokea. *(Makofi*)

Kwa sababu iko siku maji pale yatamwagika Buzwagi tutapata dharura ya kwenda kutafuta vyanzo vya maji, ipo siku wananchi watapata shida Wilaya ya Bukobe ndiyo tunaingia kwenye dharura.  Kwa hiyo, nashauri Serikali iendelee kutenga maeneo kwa haraka kama ambavyo Mheshimiwa Waziri ameanza kuchukua jitihada, aende nazo kwa kasi.

Baada ya kusema hayo, sikuwa na mengi sana ya kuchangia, lakini niipongeze sana Serikali kwa jinsi wanavyoendelea kuchukua hatua na yale niliyoshauri wayafanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi*)

**MHE. CHARLES N. MWERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote, nianze kuungana na Watanzania na Waheshimiwa Wabunge, kuipa pole Familia ya Mheshimiwa Kawawa, alikuwa Kiongozi mwadilifu katika nchi hii.

Vilevile ninawashukuru Wananchi wangu wa Tarime, kwa ushirikiano mkubwa ambao wamekuwa wakinipa wakati ninapotekeleza uwakilishi wangu hapa Bungeni, pamoja pale Tarime. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru sana Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, kwa kazi na taarifa nzuri ambayo wameitoa hapa Bungeni. Taarifa ni nzuri, nafikiri Serikali ikiisimamia na kuitekeleza, itakuwa imewasaidia Watu wa Nyamongo. Pamoja na hayo, nitoe masikitiko makubwa kwa Serikali kwa jinsi inavyolishughulikia suala la North Mara; halingehitaji kwamba mpaka tupate Taarifa ya Bunge ili mambo yaweze kutekelezwa pale. Kuna mambo ya msingi ya haraka ambayo yalitakiwa yafanyike pale. Hii ilikuwa ni dharura ambayo ilitakiwa ishughulikiwe mapema iwezekanavyo, lakini katika agizo la kwanza, Serikali inaposema kwamba haikuwa na fedha za kufanya uchunguzi wa kina kuangalia madhara ambayo yametokana na *chemically* ambayo imeingia Mto Tigite, nashindwa kuelewa! Serikali kweli inashindwa kupata fedha kwa ajili ya kufanya shughuli za kuleta utafiti wa haraka na kutoa majibu? Hata kama tungeweza kuchukua fedha kidogo ya EPA, ingeweza kushughulikia wananchi pale Nyamongo. *(Makofi*)

Mimi nisikitike kwamba, hilo kwa kweli halijaweza kufanyiwa kazi na nilifikiri kwamba, hili la kwanza ambalo lingefanyika kujua kama ile *chemically* ambayo ilikuwa inaingia katika Mto Tigite ndiyo iliyosababisha wananchi na mifugo kufa. Kwa elimu ya kawaida tu, tindikali ambayo ni *sulphuric acid* inaingia Mto Tigite pale kuna madhara ambayo yanatokea kama mimba kutoka na kuhara. Sasa unapoangalia kwa taarifa ambazo ninazo, jana nimeongea na Mheshimiwa Diwani wa Kata ile na ametoa taarifa kwamba, hata wale watu waliochukuliwa *sampuli* za damu pamoja na mifugo wale tayari walishakufa.

Kwa kweli inasikitisha sana na taarifa ambayo ninayo katika Vijiji vya Nyarwana, Wegita na Nkerege, bado wananchi wanakufa, mifugo inakufa, lakini Serikali inasema imechukua hatua; hatua gani ambazo zimefanyika? Hatua ambazo zingechukuliwa ni kuhakikisha binadamu hawafi pale. Kila siku mimba zinaharibika pale, lakini Serikali inasema imelifanyia kazi. Kwa kweli nilikuwa ninaiomba Serikali katika hili, taasisi maalum au ya binafsi au ya kimataifa, iweze kuhusishwa ichukue sampuli ilete majibu sahihi kwa sababu nimekuwa nikiona pengine Serikali inakuwa inaegemea sana upande wa mwekezaji.

Suala lingine ambalo ningependa niliongelee ni kuhusu uchafuzi. Wananchi wapewe shilingi milioni 250 kama Waheshimiwa waliotangulia kuongea walivyosema. Shilingi milioni 250 ni pesa ndogo, ambazo nafikiri hilo zoezi lingekuwa limeshaanza. Mpaka sasa wananchi wale bado wanaendelea kutumia yale maji na madhara bado yanaendelea kuongezeka. Kuna madini tembo, *heavy metal*, mfano, *zinc, magnesium,* bado zinaingia mle ndani na madhara bado yapo, lakini ukiangalia kwenye ripoti hii inaonekana kwamba, yale madini tembo yako sawa katika vipimo ambavyo ni vya kawaida; ndiyo maana nilikuwa naiomba nikiiagiza Serikali ilete chombo ambacho kitaleta imani kwa Wananchi wa Nyamongo na Kibasuka. Kuna suala la

wachimbaji wadogo, Waziri wa Nishati na Madini, tulifanya naye ziara pale Nyamongo, amekuwa akiahidi wananchi lakini lini hilo litatekelezwa? Kila wakati itakuwa ni kutoa ahadi.

Ahadi hiyo lazima itekelezwe ili pawepo na amani, wananchi wakienda kuangalia kidogo mabaki pale, polisi wanatupa risasi tu na kuua wananchi wangu wasiokuwa na hatia. *(Makofi*)

Tunaiomba Serikali ihakikishe kwamba, Wananchi wa Nyamongo wanapewa maeneo ya kuchimba. Serikali ilifanya makosa makubwa kuingia mikataba ambayo haimsaidii Mtanzania wala haimsaidii Mwananchi wa Nyamongo. Wananchi wa pale ni maskini na mikataba hii ipo kwa manufaa ya mwekezaji. Sasa tuitake Serikali iwape wananchi wale maeneo ya kuchimba ili amani iweze kuwepo, bila hivyo itakuwa ni vita ya kupigana mara kwa mara. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, ningependa kuongelea kuhusu fidia. Mgodi kweli upo, lakini inatakiwa wananchi waweze kulipwa fidia ili waondoke kwenye maeneo yale na ule mgodi umejengwa katika makazi ya wananchi. Sasa siweze kumwambia mwananchi aondoke akafanye shughuli nyingine kabla hajalipwa. Kwa hiyo, tuhakikishe wananchi wale wanalipwa fidia ili mwekezaji aweze kufanya kazi zake vizuri zaidi. Tutasema kwamba, Serikali inachukua hatua za kuweka mazingira, lakini mpaka sasa wananchi hawapati huduma ya maji safi pale. Kwa hiyo, naiomba Serikali ihakikishe kwamba, wananchi wote ambao wapo katika maeneo ya mgodi wanalipwa fidia ambayo inalingana, kwa sababu pale chini kuna dhahabu. *(Makofi*)

Utakapomwambia mwananchi kwamba, unamlipa pesa kidogo, hawezi kukubaliana. Kwa hiyo, ni lazima pawepo na mazungumzo kati ya Serikali, Mwekezaji na Wananchi ili waweze kukubaliana, mwananchi aweze kulipwa haki anayostahili. *(Makofi*)

Kuhusu suala fidia kwa wahanga ambao walishafariki, mifugo imekufa, basi tuweze kujua ni nani anayewajibika kwa hili; kama ni Serikali itawajibika maana Serikali ndiyo iliyoingia mikataba na huyu mwekezaji. Kama mwekezaji haaminiki, Serikali ilikuwa wapi kipindi chote; Uongozi wa Wilaya ulikuwa wapi; Uongozi wa Mkoa ulikuwa wapi? Tunapokuwa tunalitoa hili, unakuta Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya anakwambia ni mambo ya kisiasa; sasa unajiuliza mambo ya kisiasa yanatoka wapi katika uhai wa mwananchi? Kwa mfano, mwananchi aliyekuwa pale alikuwa ni Diwani wa Chama cha Mapinduzi na ndiye aliyesema kwamba, kuna hali mbaya ya uchaguzi, lakini kiongozi unapomuuliza anasema ni mambo ya siasa; mambo ya siasa yanatoka wapi? *(Makofi*)

Waziri wa Mambo ya Ndani alikwenda pale akadanganywa kwamba, kuna uvujaji wa kemikali zinaingia Mto Tigite, lakini ni hatua gani zimechukuliwa? Waziri alikuwepo pale lakini hakuchukua hatua yoyote ya utekelezaji. Inawezekana Kamati ikawa inatoa taarifa nzuri na imeiagiza Serikali ilisimamie, lakini katika kulifanyia kazi tumeambiwa historia tu. Tunatakiwa hili jambo lifanyike na hao Watu wa Nyamongo nao waonekane kwamba wanaishi Tanzania hii.

Kwenye Kamati kuna kitu kimoja ambacho hawakukisema kuhusu polisi na linajitokeza sana. Tulipotembelea pale, polisi walitumia muda mwingi kupambana na wananchi na wamekuwa wakiwaua Wananchi wa Nyamongo ambao hawana hatia. Ukiongea na mwekezaji anakwambia si ni Mapolisi wa Tanzania, polisi wenu ndiyo wanaoua. Juzi tu tarehe 2, Mwita Matiku aliuawa na polisi kwa kupigwa risasi ya kichani; ni jambo la kusikitisha sana namna

Serikali isivyojali wananchi wake; mwananchi anapigwa risasi anatoa taarifa Serikalini *no action*! Wananchi wa Nyamongo na Tarime tumechoka kuuliwa na polisi wakati tuko katika nchi yetu na hatuwezi kuvumilia hilo. Tunataka Serikali ichukue hatua na kwa vile Waziri Mkuu yuko hapa ananisikia, hatua za kisheria zichukuliwe na polisi ambao wamekuwa wakiwaua wananchi ambao hawana hatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru lakini niseme kwamba, Serikali iyafanyie masuala haya na taarifa zipatikane. La sivyo, nimwombe Waziri wa Jinsia na Watoto atembelee akinamama wa maeneo ya Kibasuka, akaone jinsi gani madhara yametokea kwa akinamama hao.

Baada ya kusema hayo, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. ALI KHAMIS SEIF**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia juu Taarifa ya Kamati ya Maliasili na Mazingira. Niseme kuwa, mimi ni Mjumbe wa Kamati hiyo; ni dhahiri kuwa, imegundulika hapa Bungeni kuwa kwenye Mgodi wa North Mara kuna uchafuzi mkubwa wa mazingira. Ninadhani Serikali imekubali hilo, kwa hiyo, hilo halina mjadala.

Sasa labda nijaribu kueleza kwa mtazamo wangu ilikuwaje tukafikia katika hali hiyo; ninadhani hilo ndiyo umuhimu zaidi, kwa sababu ukiiangalia Taarifa hiyo, tayari marekebisho yameshafanyika kiasi cha kuridhisha, lakini tuone kwa nini tukafikia katika hatua hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninahisi kuna mambo matatu yametokea, ambayo ndiyo yaliyotufikisha hapo ikabidi vyombo vya habari na taasisi za dini wapige kelele kuhusiana na hali za wananchi katika eneo la North Mara.

Jambo la kwanza ni Serikali kupuuza mchango wa Wapinzani katika Bunge kuhusiana na jambo hili. Suala hili kwangu mimi naliona ni la mwanzo na nitalitoa maelezo zaidi hapo baadae.

Suala lingine ni watendaji kutotilia maanani toka ngazi za Wilaya, Mkoa na hata Kanda; hawakutekeleza wajibu wao ipasavyo.

La tatu ambalo ninahisi limetufikisha hapo, inaonekana mwekezaji hajali mazingira, anachojali yeye ni kupata zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaposema Serikali inapuuza au kudharau michango ya Upinzani ni kwa sababu hata zikiangaliwa Hansard za Hotuba za Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, kuitanabaisha Serikali juu ya suala zima la uchafuzi wa mazingira katika Mgodi wa North Mara mfano, katika hotuba yake ya mwaka 2007/2008, Serikali haikujali. Ilisemwa mle kuwa, Mto Tigite upo katika hali mbaya, lakini ikaonekana kwa sababu waliosema ni Wapinzani basi hawa kazi yao ni kupinga tu. Tulirejea tena katika maelezo ya Hotuba yetu ya mwaka 2008/2009, kueleza wasiwasi kuhusiana suala zima la mazingira katika Mgodi wa North Mara, lakini kwa sababu ni Wapinzani, basi Serikali ikanyamaza kimya. Kwa hiyo, pale ambapo vyombo vya habari na taasisi za kidini zilipotoa habari na habari ile ikapokelewa na Kamati ya

Ardhi, Maliasili na Mazingira na pengine ingepokelewa na Wapinzani, yangelikuwa hayo hayo, ikaonekana ni wakati muafaka wa kuchukua hatua. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kuwa, sisi Wapinzani ni Watanzania, tuna imani na nchi hii, kwa hiyo, tunapoeleza yetu ni vema Serikali itafakari, ichunguze na itekeleze yale ambayo sisi tumeyasema. Hatuwezi kukaa hapa watu wazima tukasema mambo ambayo hayapo na hata Kanuni za Bunge haziruhusu kusema uongo. Ninahisi hili ndiyo lililosababisha hali yetu ikafika hapo ilipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni Watendaji. Kamati ndogo iliyoundwa na Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira na Nishati na Madini ilikwenda kule, ni jambo la kusikitisha; utafikiri kule hakukuwa na Serikali. Utakuta kuna rundo la mawe ambayo yanazalisha zile tindikali; hivi kweli atoke Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) Dar es Salaam eti akaseme rundo lile liondoshwe wakati kuna Watendaji katika Wilaya, Mkoa na Kanda? Hivi kweli Waziri wa Nishati na Madini atoke Dar es Salaam aseme rundo lile la miamba inayozalisha tindikali liondolewe wakati kule kuna wahusika ambao wapo katika Kanda ile? Kwa hiyo, inaonekana kama Watendaji kule walikuwa katika likizo, kila unayemuuliza kwa hajibu lolote; huo ni ukweli ambao tumeugundua sisi. *(Makofi*)

Sasa Serikali kufanya kazi katika mtindo huo, hatutofika mahali popote. Hivi sasa hali imeshakuwa nzuri, lakini kwa tabia hii ya kungoja mpaka Makao Makuu ifanye kazi kutakuwa hakuna maana ule mgawanyo wa madaraka kutoka Taifa, Mkoa na Wilaya. Kwa hiyo, ushauri wangu ni kuwa, sehemu kubwa ya uharibifu wa mazingira kule ungeliwezekana kuondoshwa na Watendaji wa Wilaya, Mkoa na Kanda. Lingefanyika hilo, basi yasingetokea hayo ambayo yamejitokeza. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la tatu kama nilivyoeleza ni kuwa, inavyoonekana kwa kiasi fulani mwekezaji hajali maisha ya watu pale; anajali kupata faida! Kutunza mazingira kuna gharama, sasa unapoamua kutunza mazingira na wewe mzalishaji ni mtafutaji faida, nafasi ya mazingira itakuwa ni ndogo kwa sababu faida yako itapungua. Kwa hiyo, nadhani ipo haja ya kuona kuwa tunasimamia vizuri mambo ili mambo haya yasitokee tena. Niseme kitu kimoja, mwekezaji anawaangalia wananchi wakoje au wenye taasisi wakoje, akiona sisi tuko legelege, Watendaji wa Wilaya, Mkoa, Kanda na Serikali Kuu wako legelege na yeye atazembea hivyo hivyo. Tulipokwenda Kamati yetu ya Pamoja ya Bunge na Serikali imeoneshwa kuwa, asilimia 80 ya masuala ambayo yalihitaji muda mfupi kutekelezwa ameyatekeleza. Sasa mwekezaji ni huyu huyu, lakini kilichobadilika ni utendaji tu, kwa hiyo, ninadhani ipo haja ya Serikali kuliona hilo na kulisimamia ipasavyo. *(Makofi*)

Mheshimiwa mwenyekiti, ukiachana na tatizo la mazingira, niseme kuwa pale pana tatizo la kiuchumi; eneo lile kihistoria ni la wachimbaji wadogo wadogo. Kuondoshwa katika eneo lile hawana shughuli nyingine za kuweza kuwaendesha kimaisha. Mazingira yamedhibitiwa, lakini nasema kama Serikali haikulitatua haraka suala hili la wachimbaji wadogo wadogo, pale kutatokea matatizo siku zote halafu itabidi isemwe tu Watu wa Tarime wakaidi, lakini ukweli ufumbuzi wa hilo ni utatuzi wa wachimbaji wadogo wadogo kupatiwa eneo. Nimesikia hapa kuwa, Serikali imeshajiandaa imeshatenga maeneo, lakini kuna mchakato mwingine, kwa hiyo,

huu mchakato usije kuwa mkubwa kwa sababu kwa muda mrefu wananchi wamekosa maeneo ya kujizalishia ili kupata maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninasema maafa yanahitaji uchunguzi wa kitaalam ili kubaini afya za wananchi. Vile vile Serikali ione umuhimu wa kutenga fedha za kufanyia uchunguzi kwenye maneno haya ili mambo haya yaishe.

Mimi ninadhani hapa ipo haja ya Serikali kuona haya tunayoyasema, itenge fedha tufanye utafiti wa kina na ripoti itoke. Kama athari hiyo imetokana na mgodi au uchafuzi wa mazingira au kama ni hali halisi ya eneo lile imesababisha hayo itaonekana na Serikali itakuwa pazuri.

Mchango wangu ni huo, ahsante sana. *(Makofi*)

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge, kutokana na mwenendo unavyokwenda na hizi shughuli ambazo zimezidi, nitamwita mchangiaji mmoja tu wa mwisho kabla sijairuhusu Serikali nayo iweze kutoa mchango wake ili tuweze kuimaliza hii hoja na kuziruhusu hizi za *TICTS* na *RITES* ziweze kuingia.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Taarifa ya Kamati. Kwanza, niseme kwamba, mimi ni Mjumbe wa Kamati hii na bahati nzuri nilikuwa kwenye msafara huo; kwa hiyo, kwa mara ya kwanza na mimi nimekwenda kuona migodi, kwa hiyo, naifahamu Taarifa hiyo na ni miongoni mwa Wajumbe walioiandaa. Ninampongeza sana mtoa hoja, Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, kwa taarifa yake nzuri aliyoisoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Wizara ya Maji, kwa juhudi kubwa waliyoifanya, kutafuta maji mbadala kwa ajili ya kuwasaidia wananchi hao, kwa sababu kusingekuwa na maji mengine, wananchi wangepata madhara mengine kutokana na maji hayo ambayo walikuwa wanayatumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema tatizo kubwa la migodi ni wakati wa utafiti; watafiti wanakwenda kupima eneo kubwa bila wananchi kujua na kutafuta leseni ya maeneo makubwa unakuta wananchi baadaye wanakuwa ndani ya eneo la mgodi. Sasa wanapoanza kuchimba mgodi na kuanza kupanuka, unakuta wananchi wanaingia ndani ya mgodi. Inasemekana wananchi ndiyo wameingia kumbe hawajaingia ni wachimbaji. Kwa hiyo, katika utafiti huo, wananchi waelimishwe na wafahamishwe. Tuliliona hilo tatizo, kwa mfano, Mji wote wa Kahama uko ndani ya leseni. Sasa mikondo ya madini inakwenda kama maji ardhini na wachimbaji nao wanafuata mkondo wa dhahabu, wanafuata madini, hawachimbi sehemu ambayo haina madini.

Kwa hiyo, mkondo wa madini ukielekea kijijini nao wanakwenda wanaingia ndani ya kijiji, sasa wananchi wataambiwa hameni mpaka lini na halafu tuangalie hili tatizo la umiliki wa ardhi, ambao huku juu wanamiliki wananchi, lakini chini unaambiwa miliki siyo yako. Mtu wa madini anaweza kukuhamisha, kama umejenga jengo lako unahamishwa; kuna matatizo hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo tumeliona ni suala la malipo; ni kweli Halmashauri inalipwa dola 200,000 na kwenye Taarifa ya Waziri alionesha kwenye kitabu kwamba, Serikali wanapata dola 400,000 kwa mwezi na hii 200,000 ya Halmashauri ni kwa mwaka. Sasa ukiangalia dola 200,000 kwa mwaka na uharibifu wa mazingira na mapato yanayopatikana pale unaona kwamba ni kidogo sana. Naomba Serikali wachukue baadhi ya mapato yanayopatikana pale siyo dola 200,000 kwa mwaka, kwa sababu wananchi wanapohamishwa hawalipwi chochote hata wakilipwa hawalipwi *value* ya ardhi waliyoiacha, wanalipwa kibanda lakini value ya ardhi hawalipwi. Kwa nini wasilipwe *value* ya ardhi? Hilo ndiyo suala lingine ambalo tumeliona na ambalo ninapenda niiboreshe Taarifa ya Kamati yetu na kwa hiyo, naomba hilo lieleweke. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli maji ya Mto Tegete yameharibika, ukiangalia katika maeneo ambayo yako nje ya mgodi maji ni mazuri, hatuwezi kusema kama Taarifa ya Mwenyekiti ilivyosema kwamba asilimia mia moja ndiyo yamewadhuru wananchi, lakini kuna uwezekano mkubwa wa kukubaliana kwa sababu vijiji vilivyoko mbali hakuna madhara kama hayo? Mbona ng'ombe hawakufa? Kwa nini ikawa ni ng'ombe hawa tu ndiyo wamekufa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaweza kusema kwamba, wananchi wamedhurika kutokana na maji hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ni tatizo kubwa ni umaskini wa wananchi wanaozunguka migodi na utajiri mkubwa wa wawekezaji walioko katika migodi ile. Haiwezekani watu wakaja tu katika eneo lolote katika nchi nyingine wakawa matajiri wa kupindukia huku wanazungukwa na watu maskini, ambao mapato yanayovunwa pale wao ndiyo walikuwa wamiliki, ni nchi yao. Hapo niseme tu kwamba, nimekwenda kwenye migodi yote mitatu ya North Mara, Bulyankhulu na Geita; wananchi wanaozunguka katika migodi yote hiyo ni maskini wa kutupwa. Ukiangalia nyumba zilizoko karibu na migodi kwanza, zimepata *cracks;* na pili, zimejaa vumbi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru lakini wananchi waangaliwe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Michael Lekule Laizer. Sasa nitawaita Waheshimiwa Mawaziri watatu, lakini kwa sababu sehemu kubwa sana ninaona ilibebwa na Mheshimiwa Batilda, alipokuwa akiongea aligusa mpaka maeneo ya baadhi ya Mawaziri, sasa nafikiri ingekuwa vizuri ili kusiwe na *repetition* wawe *very brief* waje watoe michango yao.

Kwa hiyo, nitaanza na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji na mwisho kabisa atakuja Mheshimiwa Waziri wa Afya.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii. Niungane na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), kwa taarifa au maoni aliyoyatoa kufuatia Taarifa iliyowasilishwa na Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu athari za mazingira za Mgodi wa Barrick.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami pia naipongeza na kuishukuru sana Kamati ya Bunge kwa taarifa yao kuhusu kile ambacho kilitokea na hatua za utekelezaji ambazo zimefikiwa kwa sasa hivi; na ni kweli kama ulivyosema Mwenyekiti kwa usahihi, mambo mengi kuhusu maoni na hatua mbalimbali za utekelezaji ambazo Serikali imefanya, yamewasilishwa na Mheshimiwa Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Rais anayehusika na Mazingira, Mheshimiwa Dkt. Batilda Buriani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, la kwanza ni kuiunga mkono na kukubaliana na yale ambayo yamesemwa tayari na Kamati kuhusu Mgodi wa North Mara, lakini pia niseme kidogo tu kuhusu hatua za utekelezaji kwa baadhi ya mambo.

La kwanza ni kutoka kwenye taarifa yoyote halisi kuhusu utekelezaji wa baadhi ya mapendekezo na hasa kwenye sehemu ya tatu ya agizo namba mbili kwenye ile taarifa au tuseme muhtasari wa Taarifa ya Kamati. Sisi kama Wizara, tunaendelea kutekeleza ushauri ambao umetolewa na kwa kweli *Task Force* iliyopo tunaamini kwamba, itarahisisha zaidi kutufikisha kwenye lile ambalo tumelikusudia.

Sehemu ya kwanza ya agizo namba tatu inahusu utafiti unaohusisha mambo ya kiuchumi na kijamii kwa maeneo yanayozunguka migodi. Mheshimiwa Waziri wa Mazingira ameelezea, naomba nirudie tu kwamba, tunaendelea vizuri na ratiba iliyopo ni kwamba, kufikia mwezi wa tano tutakuwa tumefikia mahali pazuri zaidi katika utekelezaji wa yale ambayo tunayakusudia na kwa jinsi ambavyo Kamati imetushauri.

Kuhusu masuala ya kutenga maeneo ya wachimbaji wadogo, tumeyasema haya katika nyakati zilizotangulia lakini pia tumekuwa tukiyasema kadiri tunavyopata muda na hata hivyo kuhusu Wilaya ya Tarime tunaendelea. Maeneo ambayo ameyataja Mheshimiwa Waziri wa Mazingira, tunayafanyia kazi, lakini ambacho ninataka kusisitiza hapa na kwa sababu limejitokeza kwa baadhi ya wachangiaji ni kwamba, kabla eneo hatujalitoa kwa wachimbaji wadogo, lazima Wataalamu wa Wizara ya Nishati na Madini wajiridhishe kwamba, kwanza kuna mashapo ya kutosha ili tu isiwe kwamba tunawapa wachimbaji wadogo maeneo ambayo kwa kutegemea vifaa walivyonavyo hawawezi kuyafikia.

Kwa hiyo, hiyo imekuwa ni mojawapo ya vigezo muhimu sana ambavyo sisi kama Serikali ni lazima tuvingatie ili kutoa haki kwa sababu unaweza kutoa eneo tu lakini kumbe kwa kutegemea vifaa walivyonavyo kwa uchimbaji mdogo, hawawezi kuyafikia madini yaliyopo pale. Kwa hiyo, hiyo imekuwa ni mojawapo ya vigezo ambavyo tunavizingatia sana, lakini bahati nzuri tunaendelea vizuri na eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna mradi pia katika Wilaya ya Tarime ambao Wawekezaji wa *Barrick* kwenye Kata ya Kemambo na wengi wanafahamu hapa, wamekuwa wanashirikiana na Wananchi na Serikali, kuna mradi ambao wanaufadhili wao wenyewe Barrick kwa fedha ya Kitanzania, utagharimu kama bilioni tatu ambao kimsingi ni kwa ajili ya manufaa ya wachimbaji wadogo. Kwa hiyo, tunakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fidia kwa ujumla, tunachofahamu fidia imekuwa ikiendelea lakini kwa maeneo ya Wilaya ya Tarime imekuwa ni ya aina yake, kuna kipindi

kulikuwa na kesi ambayo ilipelekwa na walalamikaji ambao walifanyiwa tathmini kwa kutegemea Sheria iliyokuwepo, lakini walipokwenda mbele ya Mahakama, madai yao yalionekana kwamba hayatoshelezi na hatimaye Serikali ikapewa ushindi.

Sisi tunasema kwa mazingira yaliyokuwa katika Mgodi wa North Mara kutumia *Task Force* ambayo imeundwa, tunaamini kwamba tutafikia muafaka.

Kuna hili la jumla la kuwafidia wananchi ambao wanazunguka mgodi ule, ambao sasa tunasema kuna mazungumzo ambayo yanaendelea kufanyika ndani ya hii Kamati iliyoundwa na msimamizi wake wa karibu ni Mkuu wa Wilaya na sisi Serikali Kuu, pamoja na Mamlaka nyingine, tunaendelea kushirikiana ili kuhakikisha kwamba, jambo hili tunalimaliza na lisizidi kuwa kero kwa wananchi.

Sheria mpya itakapokuja na kama mnavyojua, taratibu za Bunge haziruhusu kuongelea jambo ambalo muda wake haujafika hapa Bungeni, lakini kasoro ambazo tumezibaini kutokana na Sheria zilizokuwepo mojawapo ikiwa ni Sheria ya Ardhi kuhusu fidia zitaboreshwa na hasa kutegemeana na Sheria ya mpya ya Madini ambayo tunatarajia kuiwasilisha kwenye Bunge hili ndani ya mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo na kwa kuzingatia muda, niseme yote kwa yote tunaishukuru sana Kamati kwa ushauri na maoni waliyoyatoa na sisi kama Serikali, tunaendelea kuahidi kuhakikisha kwamba, tutaendelea kutekeleza yale ambayo yana manufaa kwa taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. Sasa namwita Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia muda na mimi naomba niseme machache tu.

Labda niende moja kwa kwa moja kwenye maagizo ambayo Mheshimiwa Waziri anayeshughulikia mazingira ameyatoa.

Kwanza, nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili, Ardhi na Mazingira na Mawaziri waliotangulia kuchangia na moja kwa moja kwenye maagizo ambayo Taarifa ya Kamati imeyatoa kwa ajili ya utekelezaji wa Serikali.

Naomba nijikite kwenye agizo namba nne ambalo limegusa zaidi kwenye vyanzo vya maji. Labda niseme kwa kifupi tu kwamba, sisi tulikwishaanza kulitekeleza agizo hili tangu mwanzo, kwa hiyo, agizo limekuja likiwa kama linaendeleza tu mwendelezo wa utekelezaji, tayari tumekuwa na mipango ambayo tunaitekeleza. Tulishatenga shilingi milioni 137, ambazo ndizo zimefanya kazi hii ya kuainisha vyanzo vipya vya maji kwa ajili ya kutafuta vyanzo mbadala ili angalau wananchi wasiendelee kutumia maji ambayo yameathiriwa na tindikali.

Kwa hiyo, katika utaratibu ule ambao Waziri ameueleza wa visima 17 tumesema tumekadiria milioni 255/= zinatakiwa lakini fedha hizi bado ni nyingi kidogo, japokuwa Mbunge mmoja amesema siyo nyingi, fedha zinatakiwa wakati ambapo ni dharura ni nyingi kidogo lakini tumejitahidi na tayari tumetenga shilingi milioni 100/=, yaani ninavyozungumza hivi sasa ili angalau kwa fedha hizi tutekeleze kiasi ambacho tutaweza kuchimba visima kwa ajili ya wale wananchi wanaozunguka Mgodi wa Barrick.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuokoa muda, tumesema tuondoe mchakato huu wa kutafuta wakandarasi wa kuchimba visima, tutatumia DDCA, Wakala wetu wa kuchimba visima na kujenga mabwawa atakwenda kule kwa mtindo wa *single sourcing* na hilo litakuwa limetusaidia angalau kufanya kazi hiyo kwa haraka kupunguza muda wa kupata mkandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wananchi mimi ninajua kama anavyosema Mheshimiwa Lekule na Wabunge wengine ni wafugaji, kwa hiyo tumeangalia pia kwamba, wanahitaji maji ya kunywesha mifugo; kwa hiyo tayari tumefanya *design* za awali kwa ajili ya kujenga malambo, gharama ni kubwa kidogo takriban shilingi bilioni saba na zaidi lakini tumeona ni lazima tufanye kazi hii ya awali ili angalau tuendelee kutafuta fedha na kuendelea na kazi jinsi fedha zitakavyopatikana na tutakuwa pia tunamshirikisha mwekezaji kwa mtindo ule wa *polluter's principles* kwa sababu hatuwezi tukaubeba mzigo huu sisi wenyewe Serikali peke yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitaje kwa harakaharaka mambo manne ambayo nafikiri ningependa mkaelewa kwamba tutayafanya, nayo ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, tunaendelea kuimarisha Ofisi zetu za Bonde ili ziwe na uwezo wa kukagua vyanzo vya maji kila wakati badala ya kutumia mtindo huu ambao Waheshimiwa Wabunge wameuita mtindo wa zimamoto; watakuwa wanakwenda kila wakati kukagua mgodi na kuangalia athari zinazojitokeza. Kwa hiyo, tumewawezesha vitendea kazi na tunawapa Wataalamu ili waweze kufanya kazi hii kila wakati na kutupa taarifa.

Jambo la pili, Wizara ya Maji na Umwagiliaji, itaendelea kukagua migodi yote nchini siyo tu huo wa *North Mara* kwa sababu huo tayari ni fundisho, kwa hiyo, tutaendelea kuangalia migodi mingine yote ambayo iko hapa nchini ili kuangalia kama athari hizi zinaweza kujitokeza ili tuchukue hatua zinazofaa haraka.

Ninaomba nizungumzie kuhusu alilolisema Mheshimiwa Ruth Msafiri kuhusu wawekezaji kunyang'anya hati za kumiliki maji au kuchukua vyanzo vya maji. Mimi ninaomba niseme kwamba, Sheria Namba 11 ya 2009 tuliyoitunga hapa mwaka jana inayohusu Rasilimali za Maji, inawapa wananchi haki za kutumia maji na Sheria hiyo siyo kwa ajili ya wananchi tu wala kwa ajili ya wawekezaji tu. Kwa hiyo, Mwekezaji akija bado naye anabanwa na Sheria hii hii, ikibidi naye atafute chanzo kingine ili aweze kupewa hati ya kutumia maji. Kwa hiyo, Sheria hii itawabana wote wawekezaji na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwa harakaharaka, jambo lingine ambalo tutalifanya ni kutoa Elimu kwa wananchi kuhusu vyanzo vya maji na kuhusu uchafuzi kwa sababu siyo mwekezaji tu anayeweza kuchagua, hata wananchi wenyewe wana sehemu yao.

Kwa hiyo, hilo nalo tutaendelea kulifanya kama ni sehemu yetu ya kutekeleza utaratibu wa kuwafundisha wananchi na wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, ninaomba niseme kwamba, sisi tumeliangalia jambo hili na limetupa fundisho kwamba, ukitazama yale madini tembo yamezagaa, hatuwezi tukasema moja kwa moja kwamba ni mwekezaji tu ndiye kayaleta, mengine yanatokana na ardhi iliyopo pale, yaani miamba. Kwa hiyo, tumesema sisi kama Wizara tutafanya utafiti zaidi katika sehemu zote zile mpaka katika Wilaya ya Tarime, kuangalia uwepo na jinsi tunavyoweza tukadhibiti matatizo yanayoweza yakatokana na Madini haya yaliyopo chini ya ardhi yanayoweza kuathiri vyanzo vyetu vya maji, hapo tutakuwa tunasaidia siyo tu uharibifu unaotokana na mwekezaji na wananchi, isipokuwa itatupa picha kujua maji yetu tuliyonayo yanaweza tukayatumia vizuri namna gani.

Labda la mwisho kabisa ni hili la kufanya tathmini ya mazingira, ambalo Kamati imesisitiza sana na hili nakubaliana nalo na ninaomba niseme tunakubali kabisa kwa sababu hili ni tahadhari kubwa kwa ajili miradi yote tunayoipanga ya ujenzi wa malambo na kuchimba visima vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa harakahara kwa kweli muda ni mfupi sana, nilikuwa naweza kusema mambo niliyoyasema lakini nimalizie hapa. Ahsante sana na ninaomba kuunga mkono Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji. Sasa namwita Mheshimiwa Waziri wa Afya.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja hii ambayo ninaiunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na wachangiaji wawili; Mheshimiwa Charles Mwera na Mheshimwa Ali Khamis Seif, ambao walichangia suala la afya. Mheshimiwa Mwera alisema sampuli nyingi zimechukuliwa za maji na damu lakini majibu hatujayaona na madhara ya afya yanaendelea; watu wanaendelea kuhara, mimba zinatoka, ngozi zinababuka na watu wanaendelea kufa. Itafutwe Tume Huru ya kuchunguza madhara haya ili kurudisha imani ya wananchi kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, sampuli za damu ni kweli tulichukua na majibu yapo na tunaweza tukampatia Mheshimiwa Mwera, lakini vilevile yamo katika kitabu hiki. Mambo yote yaliyofanyika katika suala la afya yako kuanzia ukurasa wa 21 mpaka 41, anaweza akajiridhisha pale.

Vilevile katika ufuatiliaji ambao tumeendelea nao, inaonekana magonjwa yanapungua. Nina jedwali hapa nitalisoma harakahara; kuharisha mwezi Julai ilikuwa 87 ikapungua mpaka 68, 52, 47, 23, 21 mwezi Desemba na matatizo ya ujauzito mwezi Agosti ilikuwa 20, 19, 19, 10, 3 na tuelewe kwamba, haya magonjwa siyo lazima yawe yanatokana na mambo ya kemikali, maana yako katika maeneo mengine ya nchi. Hapa siyo kwamba tunapinga Taarifa yake, hii inatuambia tu kwamba tuzidi kutafuta nini kinajili katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri vilevile katika maagizo ya Kamati, agizo la kwanza linahusu afya na ninadhani ni sahihi kwamba, afya ya wananchi ipewe kipaumbele cha kwanza. Hapa inasema agizo halijatekelezwa na hii siyo sahihi sana. Sisi tuliposikia tu tarehe 25 tukawaagiza watuletee sampuli, lakini siku tatu baadaye tukapeleka Wataalamu wa Binadamu, Udhibiti na Ufuatiliaji wa Magonjwa, Kitengo cha Dharura na Maafa, Wakemia na Watu wa Maabara wakaenda kule Tarime kuwahoji watu. Kilichojionesha ni kwamba, watu wa kule hawatumii sana huduma za afya kwa sababu *record* za vituo vya afya hazikuonesha hawa watu walitibiwa pale au walifia katika hivyo vituo. Lakini jinsi ufuatiliaji na uragibishi unavyoendelea, hiyo ina-*mprove*.

Vilevile tuna Mkakati Maalum wa kuimarisha vituo hivyo ambavyo vinazunguka mgodi, ambapo sasa hivi unaendelea ukarabati wa majengo katika Kituo cha Afya cha Narwana na Zanahati ya Nyangoto, tumekarabati nyumba mbili za wafanyakazi katika Kituo cha Afya cha Nyangoto, tumefunga umeme katika Kituo cha Afya cha Nyangoto na pesa za ziada kwa ajili ya madawa zimetumwa. Pia tumeazima watumishi ili kukiimarisha Kituo cha Afya cha Nyarwana na Ngamongo.

Vilevile tumeiagiza Halmashauri ya Wilaya ya Tarime walete maombi halisi ya mahitaji ya watumishi na tumeahidi kuwapelekea. Kwa hiyo, Wizara inaendelea na kuchunguza mwenendo wa magonjwa na hili ni zoezi la kudumu. Jana timu nyingine imekwenda ambayo inaongozwa na mtaalamu wa magonjwa ya ngozi.

Kwa mipango ya baadaye, tumetenga fedha kwa mwaka ujao wa fedha, kwa ajili ya uchunguzi wa kina na vilevile ufuatiliaji na uimarishaji wa Vituo vya Nyangoto na Nyarwana na Zahanati ya Nyamongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya kuoanisha matatizo tunayoyaona na magonjwa ni kitu ambacho kinahitaji utaalamu wa hali ya juu, kwa sababu magonjwa yote tuliyoyataja yanapatikana nchini kote. Tunachotaka kujiridhisha ni kwamba, haya yaliyotokea na tukio hili la tindikali kuna uhusiano wa namna gani, hiyo ndiyo itatupa njia ya namna ya kuyadhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Afya na sasa nimwite mtoa hoja ili naye aweze kumalizia hoja yake.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI – (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa michango mizuri iliyotolewa na Waheshimiwa Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge.

Kwa harakaharaka tu, ninapenda kuwatambua Waheshimiwa waliochangia kwa maandishi ambao ni Mheshimiwa Dkt. George Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Hemed Hemed, Mheshimiwa Charles Mwera, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa na Mheshimiwa Yono S. Kevela (Mb).

Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Charles Mwera, Mheshimiwa Ally Khamis Seif, Mheshimiwa Dkt. Batilda Burian, Mheshimiwa William M. Ngeleja, Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza na Mheshimiwa Prof. David H. Mwakyusa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwamba, wote waliochangia wamezungumzia maeneo yale yale makubwa ambayo na sisi kwenye Kamati tuliyataja; mambo ya fidia kwa wananchi, mambo ya uhusiano, umakini wa utendaji kazi wa upande wa mwekezaji na Serikali yenyewe, matumizi ya nguvu ya dola pamoja na utekelezaji wa maagizo ambao tunautegemea Serikali itatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo yaliyotolewa na Mawaziri wanaohusika hapa yanaonesha vilevile kwamba, kuna nia ya kutaka kuhakikisha kwamba, yale tuliyoagiza au kupendekeza yafanywe yatafanywa. Maelezo yaliyotolewa na Wizara ya Afya, Wizara ya Maji na hata Wizara ya Madini, yanaonesha kweli wana dhamira na maeneo ambayo wametamka kiasi cha fedha watakachotumia na mchakato mzima utakaotumiwa katika kutekeleza hayo. Kuna maeneo mengine, inawezekana kiasi cha fedha kitakachotumika bado hakijatathminiwa kwa sababu ya kutokupatikana kwa taarifa fulani.

Mimi ninapenda kuamini na ni mategemeo ya Kamati kwamba, kwa mwelekeo huu Wizara husika au Serikali kwa ujumla watayatekeleza haya. Nisisitize tu kwamba, tuombe wenzetu wa Serikali wawe makini na taarifa, tumeomba wazilete kwa Kamati tusije kesho tukaanza kuulizana tena kwamba hili halikuweza kutekelezwa.

Suala la fedha kwa mfano, mimi nasisitiza wamtumie mwekezaji, mwekezaji anahusika na athari zile kwa sababu angefanya EIA athari zile angegharamia yeye. Kwa hiyo, athari zinazojitokeza nyingi zinatokana na mgodi kuwepo pale na angekuwa amefanya EIA angewajibika kuzitekeleza yeye. Kwa hiyo, Serikali isione haya kumhusisha mwekezaji katika kugharamia gharama hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mheshimiwa Waziri wa Afya kuhusu agizo namba moja ambalo tumesema halikutekelezwa, tutakuwa tunamaanisha utekelezaji wa Desemba. *Report* tuliyopewa wakati ule wakati tunafanya tathmini ya utekelezaji tuliambiwa na waliokuja kuleta maelezo na *Report* iliyotolewa kwamba, walishindwa kufanya utekelezaji wa utafiti huo kwa sababu bado kulikuwa hakuna fedha. Inawezekana Mheshimiwa Waziri baada ya pale kuna vitu kwa vyovyote vimeendelea kutekelezwa mpaka leo na juhudi unazozisema hapa zinakaribishwa ninadhani zina maana hiyo. Kwa hiyo, sidhani kama kuna kupingana kwa namna yoyote ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeyazingatia yote yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge hapa na ninadhani Mawaziri wamesikia tuna imani kwamba watatekeleza wajibu wao na tutaendelea kufuatilia kama Kamati kupitia report watakazozitoa kuhakikisha utekelezaji unakuwa ni wa umakini. Naamini kabisa kama Kamati tutawajibika na kufuatilia kwa nguvu kabisa kuhakikisha kwamba ahadi tulizozitoa hapa kama Kamati na kuitaka Serikali itimize wajibu wake tunaamini kabisa itatekeleza hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo mafupi, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa kuwasilisha taarifa hiyo ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira; na kwa kuwa Bunge zima linakupigia makofi, inaonekana kimsingi watakuwa wamekubali.

Bunge limeikubali na kuipokea Taarifa ya Kamati yako. Ninakushukuru sana kwa kuweza kuiwasilisha hapa pamoja na majumuisho uliyoyatoa.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijasitisha shughuli za Bunge za asubuhi, ninapenda kuwatangazia Wabunge wa CCM kwamba, mnatakiwa muwepo katika Ukumbi wa Pius Msekwa mara baada ya kuahirishwa kwa ajili ya shughuli nyingine ambazo zitakuwa zimepangwa huko kwenye Kikao.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati wa kusitisha shughuli za Serikali asubuhi, ofisi ilikuwa imetoa Orodha ya Nyongeza ya Shughuli kwa mchana huu na orodha ya nyongeza ya shughuli ilikuwa inaonesha kwamba, kutakuwa na Hati za Kuwasilisha Mezani na hati hizo zilikuwa ni zifuatazo: Hati ambayo ingewasilishwa na Kamati ya Miundombinu kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Shirika la Reli Tanzania uliofanywa na Kampuni ya RITES; na pia hati nyingine ambayo ingewasilishwa na Kamati ilikuwa ni ile ya Kamati ya Miundombinu ambayo ingehusu Taarifa ya Utendaji wa Kazi Usioridhisha wa Kampuni ya TICTS.

Waheshimiwa Wabunge, ninasikitika kusema kwamba, taarifa hizi zote haziko tayari. Kwa hiyo, kama hazijawasilishwa maana yake ni kwamba, hakuna cha kujadili. Kwa maana hiyo, ninapenda kuahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 11.03 jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano,*
*Tarehe 10 Februari, 2010 Saa Tatu Asubuhi)*